

**KUCHUNGUZA ATHARI YA MATAMSHI YA LUGHA YA KIJITA
KATIKA KUJIFUNZA LUGHA YA KISWAHILI**

JOSEPH ISMAIL MASASA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA
MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI YA (M. A KISWAHILI - ISIMU)
YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia saina hapa chini anathibitisha kuwaameisoma tasnifu hii yenye mada **“Kuchunguza Athari ya Lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili”** na kwamba nimeridhika kuwa tasnifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili [M. A Kiswahili - Isimu] ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....
Dkt. Anna M. Kishe

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKI MILIKI

Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kukaririwa,kunakiriwa,kuhifadhiwa kwa njia yoyote iwayo au kuhawilishwa kwa mbinu yoyote ile, ya kieletroniki,kunakiri, kurudufu katika hali yoyote bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au kurugenzi ya tafiti,uchapishaji na shahada za uzamili ya chuo kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

TAMKO

Mimi, Joseph Ismail Masasa natamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii iitwayo Kuchunguza athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili ni kazi yangu mimi mwenyewe, nakwamba haijawahi kuwasilishwa popote pale kwa lengo la kutunukiwa shahada kama hii au yoyote ile iwayo.

.....
Saini

.....
Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia kwa wanangu wapendwa Rhoda, Masasa, Abdi na Nyakaji pamoja na mke wangu mpendwa Mariamu Joseph.

Pia naitabarukia wazazi wangu Masasa na mama yangu Mpendwa Rhoda Chiraka ambaye sasa ni marehemu na kwa wanafunzi wote wa kiswahili Isimu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

SHUKURANI

Mwanzo kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenisaidia na amenibariki katika kufanikisha kazi yangu hii. Kama inavyojulikana, mshikamano wa mikono daima hutoa kazi nzuri. Kwa hiyo mafanikio ya kazi ya, “Kuchunguza athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili” yametokana na misaada ya watu mbalimbali.

Kuna watu ambao sina budi kuwataja kutokana na misaada yao mikubwa waliyonipatia. Shukrani nyingi ni kwa msimamizi wangu Dkt. Anna Kishe, kwa juhudi zake alizo nifanyia kwa kunisimamia na kuisahihisha kazi hii hadi kufikia upeo huu unaonekana. Vilevile, namshukuru Kwa kunipa Moyo ulioniwezesha kuifanya kazi hii kwa subira kubwa. Pia ninapenda kuwashukuru Wataalamu wa lugha ya Kiswahili wa Chuo kikuu Huria cha Tanzania kwa jumla, na hasa, wale wa kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii idara ya lugha na taaluma za Fasihi kwa ushirikiano mzuri waliutoa kwangu na hivyo kuniwezesha kufanikisha kazi hii.

Shukrani zangu maalumu ni kwa Walimu wangu walionifundisha Kiswahili Isimu katika Chuo kikuu Huria cha Tanzania kituo cha Mwanza ambao ni Dkt Anna Kishe, Prof. James. S. Mdee, Dkt Zeld Elisfa, Dkt Hanna Simpasa, Dkt Ligembe na Dkt Hadija Jilala kwa Moyo wao na ufundishaji wao mzuri.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu ni kujua jinsi ambavyo mtoto wa kijita anayejifunza lugha ya kiswahili anavyoathiriwa na lugha yake mama katika harakati zake za kujifunza lugha ya kiswahili sanifu. Utafiti huu umefanywa katika Wilayani Butiama. Taasisi mbili zilishilikishwa Shule ya Msingi Chimati A na Shule ya Msingi Bulinga A. Pia wataalamu (Wazazi) wa Vijiji hivyo Chimati na Bugunda. Utafiti huu umetumia mbinu ya dodoso, hojaji na mahojiano ya makundi katika kusanya data zake. Matokeo ya utafiti huu umebaini kwamba pana Athari ya Lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili Sanifu. Hii inatokana na sababu ya Watoto kuhamisha uelewa wa Lugha ya Kwanza ya Kijita kwenda Lugha ya Pili ambayo ni lugha ya Kiswahili. Watoto walio wengi wana Athari ya Lugha Mama. Mapendekezo ya Mtafiti ni kwamba lugha ya kijita inaleta athari kwa watoto wa kijita na wajita wenyewe wanapokuwa wanajifunza lugha ya kiswahili sanifu. Hivyo pana haja ya kuanza kujifunza lugha hii ya Kiswahili katika mazingira ya nyumbani. Ili awe na uwezo wa kumdu kutumia kiswahili sanifu. Mtoto wa kijita akijifunza lugha ya kiswahili tangu utotoni kutamwezesha kuimudu lugha hii ya kiswahili sanifu, na hivyo kumsaidia kumdu somo lakiswahili shuleni pamoja na masomo mengine bila ya kuwa na usumbufu katika maendeleo yake kitaaluma ikizingatiwa kwamba takribani karibu shule zote za msingi za serikali nchini wanafunzi hufundishwa kwa kutumia lugha hii ya kiswahili sanifu isipokuwa somo la kiingereza. Hivyo kwa mtoto wa kijita kuimudu lugha hii ya kiswahili sanifu tangu utotoni ni hatua mojawapo muhimu katika maendeleo yake shuleni.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....	1
HAKI MILIKI.....	2
TAMKO	3
TABARUKU	4
SHUKURANI	5
IKISIRI	6
YALIYOMO.....	10
MAJEDWALI	11
ORODHA YA VIAMBATANISHO.....	12
ORODHA YA VIFUPISHO	13
SURA YA KWANZA.....	14
UTANGULIZI.....	14
1.1 Usuli wa Mada	14
1.2 Tamko la Utafiti	18
1.3 Malengo ya Utafiti	18
1.4. Lengo Kuu.....	18
1.4.1 Malengo Mahususi	19
1.5 Maswali ya Utafiti.....	19
1.6 Nadharia Tete	20
1.7 Umuhimu wa Utafiti	20
1.8 Vikwazo vya Utafiti	20
1.8 Mipaka ya Utafiti	21
1.9 Hitimisho.....	9

SURA YA PILI.....	22
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI.....	22
2.1 Utangulizi.....	22
2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi	23
2.3 Pengo la Utafiti	32
2.4 Kiunzi cha Nadharia.....	32
2.5 Kiuzi cha Nadharia.....	32
2.6 Hitimisho.....	33
SURA YA TATU	34
MBINU ZA UTAFITI.....	34
3.1 Utangulizi.....	34
3.2 Mbinu za Ukusanyaji Data.....	34
3.3 Data ya Awali/Upili	35
3.4 Dodoso	35
3.5 Hojaji.....	36
3.5.1 Mahojiano/Usaili.....	37
3.6 Data za Msingi	38
3.7 Sampuli na Njia za Usampulishaji	39
3.8 Uteuzi wa Sampuli	40
3.9 Mkabala wa Utafiti.....	40
3.9.1 Vifaa vya Utafiti.....	41
3.9.2 Eneo laUtafiti	41
3.10 Hitimisho.....	41
SURA YA NNE.....	42

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI...	42
4.1 Utangulizi.....	42
4.1.1 Maswali ya Utafiti Yaliyoulizwa	42
4.2 Athari ya Lugha ya Kijita katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili	43
4.2.1 Kutokuelewa	43
4.2.2 Kuongeza Viambishi Visivyohitajika	44
4.2.3 Athari katika Matamshi.....	48
4.2.4 Msamiati.....	50
4.3 Ni Sababu Zipi Zinazochangia Kuwaathiri Wanafunzi wa Kijita Wakati wa Kujifunza Lugha ya Kiswahili	51
4.4 Lugha Nyingi katika Jamii	52
4.4.1 Mukstadha	53
4.4.2 Tatizo la Kiswahili Shuleni.....	56
4.5 Jinsi ya Kupunguza Athari za Lugha ya Kijita Wakati wa Kuwasiliana kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili Sanifu	56
4.5.1 Mikakati ya Kupunguza Athari.....	57
4.5.2 Matamshi ya Kiswahili	58
4.6 Kuwepo kwa Vikundi vya Kusoma na Mihadhara	58
4.7 Hitimisho.....	60
SURA YA TANO	61
MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO.....	61
5.1 Utangulizi.....	61
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti	62
5.3 Mapendekezo	62

5.4 Hitimisho.....	63
MAREJELEO	64
VIAMBATANISHO.....	67

MAJEDWALI

Jedwali Na. 4.1: Idadi ya Watafitiwa Kutomwelewa Mwalimu Wakati wa Kufundishwa kutokana na athari ya Kijita	43
Jedwali Na. 4.2: Kuongeza Viambishi Visivyohitajika	45
Jedwali Na. 4.3: Idadi ya Watafitiwa wa Hojaji uhusu Athari katika Matamshi.....	48
Jedwali Na. 4.4: Kuhusu Athari za Matamshi.....	49
Jedwali Na. 4.5: Idadi ya Watafitiwa Kuhusu Mwingiliano katika Msamiati wa Lugha	50
Jedwali Na. 4.6: Idadi ya Watafitiwa wa Athari ya Lugha ya Kijita katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.....	52
Jedwali Na. 4.7: Idadi ya Watafitiwa Waliojibu Kuhusu Lugha nyingi katika jamii	53
Jedwali Na. 4.8: Idadi ya Watafitiwa Waliojibu Dodoso Kuhusu Mukstadha.....	54
Jedwali Na. 4.9: Matumizi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi Wanapokuwa Nyumbani.....	55
Jedwali Na. 4.10: Data ya Watafitiwa Wanafunzi Kuhusu Tatizo la Kutumia Lugha ya Kiswahili Shuleni.....	56

ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanishi 1: Dodoso Kwa Walimu	68
Kiambatanishi 2: Dodoso kwa Wanafunzi.....	71
Kiambatanishi 3: Dodoso kwa Wataalamu (Wazazi) Walugha ya Kijita.....	74

ORODHA YA VIFUPISHO

L1 Lugha Ya Kwanza

L2 Lugha Ya Pili

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Sura hii ya kwanza ni sehemu ambayo inaeleza kuhusu uwanja wa tatizo,tatizo la utafiti,malengo ya utafiti,maswali ya utafiti,umuhimu wa utafiti,nadharia ya utafiti na hitimisho.Katika sura hii tunaangalia athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

Athari ya lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya Kiswahili ni tatizo linalozikabili jamii zilizo nyingi zinapokuwa zinajifunza kuongea lugha ya pili ambayo kwa muktadha huu ni lugha ya Kiswahili. Mtoto anapoanza kujifunza lugha ya pili atakumbana na matatizo mbalimbali kama vile matamshi, lafudhi na mkazo wa maneno. Tatizo hili linatokana na lugha mama ambayo ni lugha ya kwanza ya mzungumzaji wa Kiswahili. Mzungumzaji anakuwa na umilisi katika lugha ya kwanza ndiyo maana anapata shida pale anapooonea lugha ya pili kwani matamshi, lafudhi vinakuwa vimezoeleka katika lugha ya kwanza na hivyo kumuia vigumu kubadilika katika lugha ya pili ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Watoto wengi katika mazingira tofauti hasa ya vijijini wanapata shida hasa wanapoanza shule.Wengi wao wanakuwa wanaimudu lugha mama ambayo kwa muktadha huu ni lugha ya kwanza ya Kijita. Mtoto wa Kijita anayeanza shule ya msingi anapata shida ya kujifunza lugha ya Kiswahili. Kwa mtoto wa Kijita Kiswahili

atajifunza akiwa shuleni, kanisani, msikitini na katika mikusanyiko ya watu wengi hasa panapokuwa na kabila tafauti. Mazingira mengine yanayobaki anatumia lugha ya kijita. Hivyo Mtafiti amefanya utafiti kuona jinsi gani mtoto wa Kijita anayeanza shule ya msingi anavyopata shida kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu awapo shuleni, kwa kuzingatia fonolojia na isimu miundo (sintaksia) ya lugha ya Kiswahili.

Hivyo kutokana na tatizo hilo pana haja kubwa ya kufanya utafiti katika eneo hili ili kujua chanzo chake ni nini na jinsi ya kusaidia juu ya tatizo hili la kuchunguza athari ya lugha ya kijita katika matamshi wakati wa kujifunza lugha ya kiswahili sanifu. Kwa mazingira hayo mtafiti ameona kuwa kuna msukumo wa kufanya utafiti katika eneo hilo.

Lugha ya Kijita ni lugha mojawapo kati ya lugha za Kibantu. Lugha hii inazungumzwa katika mkoa wa Mara, Wilaya ya Butiama, tarafa ya Nyanja. Kwa ujumla Kijita asilia kinazungumzwa magharibi mwa tarafa ya Nyanja. Kwa mujibu wa Mekacha (2011) lugha hii ya Kijita ameiweka kanda ya ziwa Viktoria ambalo ni kundi la kwanza na ni la lugha mashariki mwa Ziwa Viktoria na ameliita kundi la ziwa. Hizi ni lugha zinazozungumzwa Mkoa wa Mara, Mashariki mwa Ziwa Viktoria. Kundi la Suguti, lugha za kikundi cha Suguti ni Kijita, Kiruri na Kikwaya. Hivyo nitashughulika na lugha ya Kijita asilia tu.

Utamaduni wa Wajita wanalima kilimo cha mazao ya chakula ambayo zao lao kuu la chakula ni mhogo, viazi vitamu, mahindi na mtama. Pia wanajishughulisha na biashara

ya uvuvi wa samaki katika Ziwa Viktoria. Kijita kipo cha aina moja hakina tofauti kutoka eneo moja kwenda jingine. Hivyo nimeshughulika na athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili katika taasisi mbili ambazo ziko katika kijiji cha Chimati na Bugunda. Taasisi hizo ni Shule ya Msingi Chimati A na Shule ya Msingi Bulinga A pamoja na walimu wa Shule hizo na wataalamu (wazazi) wa lugha ya Kijita katika vijiji hivyo, nimeshughulikia athari za Kiisimu. Nimechunguza kuhusu athari za fonolojia ambayo kwa mujibu wa Masamba (1996) anasema ni taaluma ya isimu inayochunguza mifumo ya sauti za kutamkwa zinazotumika katika lugha asilia mahususi za binadamu. Nao Habwe na Karanja (2004) wanasema fonolojia ni utanzu wa isimu unaochunguza jinsi sauti za lugha mahususi zinazofanya kazi katika lugha mbalimbali mahususi yaani zinavyotumika, zinavyounganishwa, na zinavyopangwa katika lugha yoyote mahususi ili kuunda tungo maneno zenye maana.

Na kwa upande wa Isimu miundo (sintaksia) Massamba na wenzake (2001) wanasema ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Kijita ni lugha mama kwa upande wa wajita. Kiswahili ni lugha ya pili kwao. Hivyo utafiti huu umeangalia mtu anayejifunza lugha ya pili. Lugha ya kijita ni muhimu sana katika jamii ya kijita kwa sababu husaidia sana katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii na pia huwasaidia kuhifadhi utamaduni wa kijita.

Maana ya lugha TUKI (2004) wanasema lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana ambayo hutumiwa na watu wa Taifa au kundi fulani kwa ajili ya kuwasiliana, kuelewana na kushirikiana katika upashanaji habari. Naye Barber (1964)

anasema lugha ni utaratibu wa kupeana ishara unaotumika katika kupashana habari kwa jamii husika. Kwa ujumla lugha ni mfumo wa sauti, ishara, nasibu, zilizokubaliwa na jamii fulani yenye utamaduni sawa kwa madhumuni ya kuwasiliana, kuelewana na kushirikiana, kupashana habari. Wataalamu waliofanya utafiti kuhusu eneo hili wakaona kuwa kuna tatizo ni pamoja na hawa:

Richard (1971) na wenzake, wamesema makosa mengi hutokana na uhamisho, kutokana na sababu walizozitoa, vipengele vya kiisimu huweza kuhamishwa kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili na hivyo kusababisha makosa katika lugha ya pili. Mtazamo wa Selinker (1960) aidha ameshabihiana na wenzake, anasema vipengele vya isimu vinavyohamishwa kutoka lugha ya kwanza hadi ya pili huathiri mfumo wa lugha ya pili. Katika utafiti huo mtafiti hajazungumzia athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ni sehemu ya kufanyiwa utafiti wangu.

Curtain (1990) katika utafiti wake kuhusu wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili anasema ni vyema waelewe misingi na miundo ya lugha hiyo na vilevile matamshi bora. Wataalamu wengine waliofanya utafiti katika eneo hili ni Cook (1969, 1971) na Ervin-Trip (1974) uhusiano uliopo kati ya lugha mbili ni muhimu kwa kuwa lugha huathiriana. Aidha wameongezea kuwa, lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Katika utafiti huo mtafiti hajazungumzia athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ni sehemu ya kufanyiwa utafiti wangu.

Mwingine ni Otiende (2013) ameshughulikia suala la athari ya lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya pili aidha aliangazia mifanyiko ya kifonolojia kati ya Kisuba na Kiswahili Sanifu, kupitia kazi yake imebainika kuwa kuna tofauti za kifonolojia kati

ya lugha hizo mbili ambazo huathiri matumizi ya lugha ya kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa kisuba. Pia amethibitisha kuwa kuna baadhi ya fonimu ambazo hutofautiana katika lugha hizo mbili na hivyo kusababisha athari katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Hawa ni baadhi ya wataalamu waliofanya utafiti katika eneo hilo kama ilivyoielezwa hapo juu. Katika utafiti huo mtafiti hajazungumzia athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ni sehemu ya kufanyiwa utafiti wangu.

1.2 Tamko la Utafiti

Tatizo la utafiti huu ni kuchunguza athari za lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili. Tunahitaji kufafanua matatizo anayokumbana nayo mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili. Hivyo utafiti huu utajadili kisha kueleza, matatizo mbalimbali anayokumbana nayo mwanafunzi wa kijita anayejifunza lugha ya kiswahili sanifu katika jitihada yake ya kuimudu lugha ya pili. Hapa tutaangalia athari katika matamshi na pia athari katika sauti. Hivyo hilo ndilo tamko la utafiti huu.

Wanafunzi wengi waliojifunza na wanaojifunza lugha ya Kiswahili kuna athari zinazojitokeza katika matamshi, uchanganyaji wa sauti wakati wa kuzungumza. Kutokana na hayo yote kuna umuhimu wa kutafiti na kubaini chanzo cha athari hizo. Utafiti huu utasaidia kubaini athari hizo na jinsi ya kusaidia kuzuia tatizokwa wale wanaojifunza lugha ya Kiswahili.

1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti yamegawanyika katika lengo la jumla ambalo ndiyo lengo kuu na lengo mahususi.

1.4. Lengo Kuu

- i. Lengo kuu la utafiti huu ni kwamba mwanafunzi ajue athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili sanifu.
- ii. Lengo kuu lingine ni kwamba mwanafunzi atambue athari za kifonolojia (Matamshi) na sauti za maneno. Isimu miundo (sintaksia) athari za kimpangilio wa kimaneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake.

1.4.1 Malengo Mahususi

- i. mwanafunzi aweze kubainisha athari za matamshi kati ya lugha ya kijita na lugha ya kiswahili sanifu.
- ii. Mwanafunzi aweze kufafanua athari za kisintaksia anapojifunza lugha ya kiswahili sanifu
- iii. Kupendekeza njia za kupunguza athari za kimatamshi na kisintaksia kwa mwanafunzi wa lugha ya Kijita anayetaka kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu.

1.5 Maswali ya Utafiti

- (i) Je, ni tofauti gani za kimatamshi zinazojitokeza kwa mwanafunzi wa Kijita anapojifunza lugha ya Kiswahili Sanifu??
- (ii) Ni athari gani za kisintaksia zinazojitokeza kwa mwanafunzi wa Kijita anapojifunza lugha ya Kiswahili Sanifu?.
- (iii) Je, njia gani zitumike ili kupunguza athari za kimatamshi na kisintaksia kwa mwanafunzi wa lugha ya Kijita anayetaka kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu?

1.6 Nadharia Tete

Kwa mujibu wa TUKI (2004) Kamusi ya kiswahili sanifu, nadharia tete ni wazo linalotokana na ukweli unaojulikana ambao hutumiwa kujenga hoja. Enon (1995) anaeleza kuwa nadharia tete ni mabunio ya matokeo tarajiwa ya utafiti unaokusudiwa kufanyika.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- (i) Athari ya lugha mama kwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya kiswahili.
- (ii) Mbinu za kusaidia kuondoa athari ya lugha mama katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu ufuatao:

- (i) Kubaini mambo yanayoleta athari kwa Wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.
- (ii) Kusaidia Wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili.
- (iii) Kusaidia kuendeleza tafiti nyingine katika lugha hii kwa Wanazuoni watakaoshughulika na lugha hii ya kijita.

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti ulipata vikwazo mbalimbali katika ukusanyaji wa taarifa zake. Kwanza utafiti ulipata shida ya usafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine katika ukusanyaji wa data. Hii ni kutokana na kuwa utafiti ulifanyika katika maeneo mawili tofauti na hivyo kumlazimu mtafiti kutoka eneo moja kwenda eneo jingine ili kuweza kukusanya data alizokuwa anazihitaji. Hivyo Mtafiti alilazimika kukodisha Usafiri wa

Pikipiki baada ya kuchoka kutembea kwa miguu kutoka eneo moja kwenda eneo jingine.

Utafiti pia ulipata vikwazo katika kupata baadhi ya vitabu vya Marejeleo ambavyo alilazimika kuvinunua kutokana na kuhitajika kwa hivyo vitabu. Kikwazo kingine ni muda ulikuwa ni mfupi mno ukilinganisha na namna ambavyo ilitakiwa kuandaa na kukusanya hizo data kwa muda muafaka ili kukamilisha utafiti huo.

1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu mtafiti amechunguza lugha ya kijita asili na kiswahili. Utafiti umeshughulika na athari za kiisimu katika matamshi ya lugha ya kijita na uchanganuzi wa mpangilio katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake katika kujifunza lugha ya kiswahili na maana ya lugha ya kiswahili na kijita kwa ufupi. Na ni kwa njia zipi kijita kimeathiri lugha ya kiswahili kwa kuzingatia zaidi nadharia ya mawasiliano.

1.9 Hitimisho la Jumla

Katika sura ya kwanza Mtafiti alitoa maana mbalimbali za vipengele muhimu alivyotumia katika utafiti huu kwa kuelezea maana ya lugha kulingana na Wataalamu jinsi wanavyoelewa maana ya lugha, maana ya lugha ya Kiswahili pamoja na lugha ya Kijita. Vilevile katika sura hii utafiti umeonesha nadharia iliyotumika katika utafiti huu pamoja na Malengo ya utafiti, Tatizo la utafiti na umuhimu wa utafiti.

Katika sura ya pili, utafiti ulihisu juu ya mapitio ya vitabu alivyosoma Mtafiti vinavyohusiana na Mada ya Utafiti yaani Vitabu vyote vilivyotumika katika tasnifu

yake, vitabu hivyo vilivyohusiana na athari ya lugha ya Kiswahili, na si katika Kiswahili tu hata katika lugha nyingine ambavyo vilizungumzia juu ya athari ya lugha. Katika sura ya tatu Utafiti ulionesha mbinu za Utafiti ulizotumia wakati wa kukusanya data. Utafiti ulifanyikia Maktabani na Mawandani. Mbinu zilizotumika katika Utafiti huu, zilisaidia Utafiti kukusanya data za Msingi na fuatizi ili kukamilisha malengo na kupata kujibu maswali ya utafiti.

Katika sura ya nne Utafiti ulichambua data ili kupata majibu juu ya maswali ya Utafiti kama yalivyoandikwa sura ya kwanza.

Na mwisho ni sura ya tano ambayo ni ya hitimisho la Utafiti huu kwa kufanya Muhtasari na Mapendekezo katika athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa vitabu vilivyoandikwa kuhusu mada ambayo unayoifanyia utafiti. Haya ni marejeo ya vitabu unavyovisoma kuhusiana na mada ya utafiti wako. Enon (1965) anasema mapitio ya vitabu ni utaratibu na uchanganuzi wa vitabu na matini mbalimbali yanayohusiana na mada inayofanyiwa utafiti. Katika sura hii Mtafiti amepitia na kuhusianisha mawazo na hoja mbalimbali kama zilivyojitokeza katika matini mbalimbali na jinsi zinavyohusiana au kukinzana na yaliyomo katika athari ya lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni kazi ya kusoma vitabu vilivyoandikwa kuhusiana na utafiti unaofanyika. Mekacha (2011) katika utafiti wake kuhusu lugha moja kuathiriwa kutokana na muktadha wa matumizi yake amebaini kuwa lugha ya Kiswahili hutumiwa hasa katika shughuli za kijamii zaidi kama vile ofisini, shuleni, sehemu za kazi, biashara na mahali ambapo panamwingiliano wa makabila mbalimbali ndipo kiswahili hutumika. Watu wanapokuwa nyumbani kwao kwa asilimia kubwa hutumia lugha zao za asili. Utafiti huu umenisaidia katika utafiti wangu ingawa haujaeleza kile ambacho ninaenda kukifanyia utafiti. Haujagusia athari katika lugha ya Kijita hivyo ndilo pengo ambalo utafiti wangu utashughulika nalo.

Kulingana na Corder (1967) yeye katika utafiti wake kuhusu nadharia ya lugha kadirifu na uchanganuzi wa makosa anasema, uchanganuzi wa makosa ni muhimu kwa sababu humwezesha Mtafiti kujua jinsi watu hujifunza lugha na mikakati wanayotumia katika harakati za kutambua lugha lengwa. Wanaojifunza hukiuka kaida za lugha ya pili. Wanafunzi wa lugha ya pili mara nyingi huhamisha usemi wa lugha ya kwanza na kutumia sheria zake katika lugha ya pili anaendelea kusema Corder (1967) anaeleza kuwa matatizo yanayojitokeza mtu anapojifunza lugha ya pili ni jambo la kawaida kutokea. Kabla ya Mwanafunzi kuzoea matumizi kamili ya kanuni ya lugha ya pili hufanya makosa hapa na pale. Corder (1967) anatofautisha makosa na matatizo yanayotokea mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili. Kulingana naye, makosa ni matatizo yanayotokana na utendaji na haya ni kikwazo chochote na yanaweza kutokea katika hali zozote. Hata hivyo makosa yanadhihirika Kwa

kuzingatia umilisi na utendaji wa lugha. Kazi yake itasaidia katika utafiti wa athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Ingawa utafiti wa Corder (1967) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Selinker (1969), yeye katika utafiti wake ameeleza mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika kuchanganua matatizo katika matumizi ya lugha. Mifanyiko hiyo ni pamoja na ujumlishaji mno kutokana na mifumo ya L1 inayotumiwa kiholela, uhamishaji wa kanuni za L1 hivyo hukiuka kanuni za L2, mikakati ya mawasiliano katika L2, njia za kujifunza zisizokuwa halisi na uhamishaji wa ufundishaji ambapo makosa hutokana na kutokuwa na umilisi kwa wanaofundisha. Kulingana naye, makosa haya yanaibua kiwango kingine katika matumizi ya lugha ambayo ni lugha kadirifu. Lugha kadirifu ni lugha inayojitokeza wakati ambapo mzungumzaji yuko katika harakati ya kujifunza lugha ya pili. Uzungumzaji wa lugha kadirifu huhamisha kanuni za lugha ya kwanza kwa lugha lengwa. Kazi hii ya Selinker itachangia katika kazi yangu kwa kuwa imeniwezesha kuyabainisha makosa kwa kutumia baadhi ya vigezo alivyovitaja. Kazi ya Selinker ya (1969) ilishughulikia lugha kwa ujumla, kwa upande wangu nitashughulikia athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili.

Selinker (1972) anaeleza kuwa mfumo huu mpya unaojitokeza unaweza kuchunguzwa kwa kushirikisha wanaojifunza lugha ya pili katika maandishi na mazungumzo. Aligundua kuwa kadri mwanafunzi anavyozidi kujifunza ndivyo matatizo yazidi

kudidimia. Kazi ya Selinker (1972) imenisaidia kuelewa mtizamo wa lugha kadirifu. Lugha kadirifu ni lugha inayoundwa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili katika harakati zao za kuimuidu lugha lengwa. Lugha kati hutofautiana na lugha ya kwanza ya mwanafunzi wa lugha lengwa. Selinker amesisitiza kwamba, mfumo huu tofauti wa kiisimu unaweza kuchunguzwa kwa kushirikisha wanaojifunza lugha ya pili katika maandishi au mazungumzo. Anasema lugha kati hubadilika badilika kulingana na muktadha. Lugha kadirifu huwa imekiuka kanuni za lugha lengwa hivi kwamba hujitokeza kama lugha kamili yenye mfumo wake wa kiisimu. Kwa mujibu wa Gas na Selinker (2008:14) kwa kutumia mtazamo wa lugha kadirifu tunaweza kuvichanganua vipengele vya lugha kama vile sarufi, fonolojia, Mofolojia, Msamiati, na semantiki. Ingawa utafiti wa Selinker (1972) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Rapando (2005) yeye katika utafiti wake alichunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi. Katika utafiti wake Rapando aligundua kwamba baadhi ya makosa yanasababishwa na lugha ya kwanza, kiingereza na Sheng. Aidha, alijumuisha mno udhihirikaji kusababisha makosa ya kimofosintaksia. Utafiti huu utanisaidia katika utafiti wangu wa athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili. Ingawa utafiti wa Rapando (2005) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Curtain (1990) katika utafiti wake kuhusu wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili, anasema ni vyema waelewe miundo na misingi ya lugha hiyo na vilevile matamshi bora. Kwa mujibu wa Cook (1969, 1971) na Ervin – Trip (1974) uhusiano uliopo kati ya lugha mbili ni muhimu kwa kuwa lugha huathiriana. Aidha wameongezea kuwa, lugha ya kwanza huathiri ujifuzaji wa lugha ya pili. Kazi ya mwandishi huyu ilinifaa katika utafiti huu kwa kuwa kazi yao ilitilia mkazo suala la mwingiliano baina ya lugha mbili na pia kwa kuangazia athari ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Kwa hiyo kazi yao imeniwezesha kuangalia athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili hivyo, ulinganisho wa sentensi za lugha hizo umechangia pakubwa katika kubaini athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili. Vile vile, kazi hiyo ilikuwa data toshelezi ya kudondoa maneno yenye athari ya lugha ya kwanza na kisha kuzioanisha ili kupata tofauti zinazojitokeza kati ya lugha hizo mbili. Ingawa utafiti wa Curtain (1990) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Richard (1971), Carroll (1971) na Swan na Smith (1987) katika utafiti wao wameshughulikia suala hili la makosa. Wamesema makosa mengi hutokana na uhamisho. Kutokana na sababu walizozitoa, vipengele vya kiisimu huweza kuhamishwa kutoka Lugha ya kwanza hadi lugha ya pili na hivyo kusababisha makosa katika Lugha ya pili. Mtazamo wa Selinker (1960) aidha umeshabiana na wa wenzake, anasema vipengele vya isimu vinavyohamishwa kutoka Lugha ya kwanza hadi Lugha ya pili huathiri mfumo wa Lugha ya pili. Ingawa utafiti wa Richard (1971), Carroll (1971) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha

ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Norrish (1983) na Brown (1977) hoja yao inakalibiana na hoja ya Selinker, wamepiga hatua na kuongezea kuwa makosa yafaa kuchukuliwa kama ishara ya maendeleo Mwanafunzi anapokuwa katika kujifunza Lugha ya pili. Aidha kwa mujibu wa Brown (2000), Corder (1973) na Larsen (1992) makosa huweza kujitokeza katika viwango vyote vya Isimu. Ingawa utafiti wa Norrish (1983) na Brown (1977) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Otiende (2013) yeye katika utafiti wake amejishughulisha na Athari ya Lugha ya kwanza katika Lugha ya pili. Aidha aliangazia mifanyiko kati ya Kisuba na Kiswahili sanifu. Kupitia kazi yake imebainika kuwa kuna tofauti ya Kimofolojia kati ya Lugha hizo mbili ambazo huathiliri matumizi ya Lugha ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Lugha ya Kisuba pia amethibitisha kuwa kuna baadhi ya Fonimu ambazo hutofautina katika Lugha hizo mbili na hivyo kusababisha Athari fulani katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kazi hii inafaa ingawa haijahusisha kipengele cha Sintaksia. Sintaksia huangazia sentensi kwa kina na sheria za uundaji wa sentensi. Pamoja na hayo kipengele hicho kimeshughulikia viambajengo anuai vinavyounda sentesi na jinsi viambajengo hivyo huathiriwa katika sentensi. Ingawa utafiti wa Otiende (2013) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza

kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Dixon (1992) yeye katika utafiti wake anaamini kuwa uhusiano wa Lugha ni kati ya Jamii husika, Wazazi, Watoto na ndugu katika Uko. Lugha inaweza kukua au kuanguka au kuathiriwa hii ni kutokana na kuwepo na matumizi ya Lugha nyingine katika Jamii hiyo. Kwa mfano kulingana na Mkude 1978, Batibo, katika Brenzinger 1992, Batibo katika Kahigi na wenzake 2000, Polome 1980, Mekacha 1993 na Ngonyani 1994, wanasema Tanzania kuna lugha za makabila idadi zinazotajwa zinaanzia 112 hadi 130. Zinapatikana katika Jamii ya Watanzania, lakini kutokana na ukuaji wa Lugha ya Kiswahili kimechukua nafasi kubwa katika Nchi ya Tanzania katika mawasiliano ya Kiuchumi na Kiutamaduni katika Mawasiliano ya kila siku. Hususani Lugha za Makabila matumizi yake kwa kiasi kikubwa zimebakia katika sehemu za vijijini tu. Watu wengi sana katika mazingira ya vijijini bado wameathiriwa na Lugha za Makabila yao hii ni kutokana na matumizi ya Lugha hizo kwa wakati mwingi. Pia anaendelea kusema kuwa, kubadilika au kufa au kuathiriwa kwa Lugha husika, hii huweza kusababishwa na shughuli zinazotendeka katika Eneo husika. Kwa mfano, mwingiliano wa shughuli za biashara, Kilimo na shughuli za Kiserikali. Ingawa utafiti wa Dixon (1992) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Rocha (2011) katika utafiti wake kuhusu Lugha asili za Makabila ya Tanzania, anasema Lugha Mama na Lugha ya pili kwa Watanzania wengi Lugha Mama ndiyo

Lugha ya kwanza kujifunza maana huzaliwa na kuikuta katika Jamii yake na Lugha ya kiswahili huwa ni Lugha yake ya pili kwa mujibu wa Watanzania wenyewe si Watanzania wote kuwa Lugha ya Kiswahili ni Lugha ya pili, wengine ni kama Lugha yao Mama maana huzaliwa na kuikuta katika mazingira yao. Hali hii imechangiwa na kupanuka sana kwa matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Nchi yetu ni wazi kuwa watu wengi wanaozaliwa Mijini lugha yao hasa ni Kiswahili hata kama Wazazi wake wanazungumza Lugha zao za Makabila. Kiasi kikubwa ambacho kimebaki kwa matumizi ya Makabila, hasa ni Vijijini maana Kiswahili hakitumiki sana kama Mijini. Kwa Watanzania wengi wanajifunza kama Lugha yao ya pili, lakini hata hivyo Lugha ya Kiswahili hutambulika kama Lugha ya Taifa katika Nchi ya Tanzania. Sababu ni kwamba Lugha hii huwaunganisha Watanzania wote maana hata shughuli za Kiserikali hutumia Kiswahili katika mawasiliona yao.

Kwa hali hiyo Lugha Mama hubakia kutumika wao kwa wao wanaoielewa Lugha hiyo kama matumizi ya Nyumbani rafiki na ndugu zake tu na vijana wanoilewa ile Lugha. Kwahiyo Lugha ya Kiswahili imechaguliwa kutumika kwa niaba ya Lugha nyingine hapa Nchini wakati wa kujifunza Lugha ya Kiswahili kama Lugha ya pili huwa tayari walishaathiriwa na Lugha zao za kwanza na kuwa wazungumzaji wa Lugha hiyo kwa muda mwingi kulingana na hali hii mzungumzaji huwa mahili kuzungumza Lugha yake tafauti na lugha ya Kiswahili. Hali hii husababishwa na misingi na kanuni za Lugha fulani maana huwa tayali mifumo yote ya utamshi wa maneno huwa umezoea kutamka maneno ya lugha hiyo lakini mzungumzaji anapoongea Lugha ya kiswahili kama lugha yake ya pili, Hujikuta anatumia kama ni za ile Lugha ya kwanza ndio maana kunakuwepo na utafauti wa kutamka na lafudhi kwa mzungumzaji. Rocha

anasema katika kipindi cha Wajerumani Kiswahili kilipewa nafasi lakini bado Athari ilibakia kuwepo.

Hata baada ya Uhuru hayati Mwl Julius Kambarage Nyerere aliteuwa Lugha ya Kiswahili kuwa Lugha ya Taifa baada ya Uhuru wa Tanganyika, ambapo hali hiyo ilichangia kukua kwa kiasi kikubwa kwa Lugha ya kiswahili kuenea kwa kasi hapa Nchini kwa upande wa Tanzania bara Kiswahili kilikuwa hakitumiki sana kama upande wa pwani ya Tanzania maana kwa kiasi kikubwa Lugha ya Kiswahili ilikuwa haitumiki sana Lugha ya Makabila ndiyo ilikuwa inatumika sana.

Richa ya kufanya hivyo lakini bado kuna Athari zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa Lugha ya Kiswahili maana kwa wengi wao Lugha ya Kiswahili huwa kama Lugha yao ya pili kujifunza ambapo kuna Athari ndogondogo zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa Lugha ya Kiswahili ndio maana kunakuwepo na utafuti wa utamkaji wa maneno ya Kiswahili na dosari hizo hujitokeza hasa katika matamshi na lafudhi ya mzungumzaji wa Lugha ya Kiswahili. Ingawa utafiti wa Rocha (2011) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kijita. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu utashughulika nalo.

Obara (2014), alifanya utafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na Wanafunzi wazungauzaji wa Lugha ya Ekegusii. Katika utafiti huo ilijitokeza kuwa makosa yanayojitokeza katika Insha za Wanafunzi hutokea katika Viwango vyote vya Usomi. Makosa haya huendelea kupungua kadri Mwanafunzi anavyoendelea katika

viwango vya Juu vya usomi. Katika utafiti huo ilibainika wazi kuwa Wanafunzi hufanya makosa haya kwa sababu ya kuhamisha mifumo ya kiisimu ya L1 kwenda kwa L2 mathalani Lugha ya Ekegusii haina fonimu /l/ na kwa hivyo Mwanafunzi anapoandika neno kama /lala/ hutumia fonimu inayopatikana katika Lugha yake ya kwanza hivyo ataandika /rara/ badala ya /lala/. Makosa haya yamekiuka kanuni za kifonolojia za Kiswahili Sanifu. Lakini ikumbukwe kuwa makosa hayawi kizuizi cha ujifunzaji Lugha ni harakati za Mtu kuimudu L2. Hivyo utafiti huo umebaini chanzo cha matokea mabaya katika Somo la Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii. Utafiti huu umeangalia L1 Ekegusii na lugha ya pili ya Kiswahili lakini bado haujazungumzia kwa upande wa lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Hivyo lengo hilo ndili litakalo shughulika nalo.

Kisakwah (2014) katika Tasnifu yake kwa ajili ya shahada ya Uzamili katika Chuo kikuu cha Nairobi. Alifanya Utafiti unaohusu uchanganuzi makosa na muundo sentensi. Ulinganisho wa Sentensi sahili za Kiswahili sanifu na za Kisuba. Katika Utafiti huo imebainika kuwa kuna makosa mengi katika insha za Wanafunzi. Makosa haya hususani huhusu vipashio vyote vya Kiisimu. Kadhalika ni wazi kuwa makosa katika tungo za Wanafunzi yakichunguzwa kwa kina, mengi husababishwa na Lugha ya kwanza. Utafiti wa Mtafiti huyo ameangalia athari zinazoletwa na makosa katika Lugha ya pili (L2) kwani zinatokana na athari ya Lugha ya kwanza (L1). Lakini bado utafiti huu haujazungumzia kwa upande wa lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Kwa hali hiyo utafiti huu utasaidia pengo hilo la lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu.

2.3 Pengo la Utafiti

Wanazuoni mbalimbali na watafiti kuhusu athari ya Lugha mama (ya kwanza) wamekuwa wakielezea mapungufu kuhusu athari ambazo zimejitokeza katika kujifunza Lugha ya Kiswahili. Japo watalaamu wengi wameangazia athari za Lugha mama katika kujifunza Lugha ya Kiswahili. Kufikia sasa hakuna uthibitisho ninao uelewa kuhusu athari ya Lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili katika Fonolojia na Kisintaksia imeshughulikiwa na hilo ndilo pengo ambalo utafiti huu umeweza kusaidia kulishughulikia ili kupata ufumbuzi wake.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Kwa mujibu wa Massamba (2004: 64) nadharia ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika msingi wa mawazo ili kutumiwa kama kiolezo cha kuelezea jambo. Naye Wamitila (2011:22) anaeleza kwamba nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kuelezea hali fulani, chanzo chake, utenda kazi wake na mwingiliano wake wa ndani na nje. Nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi ili kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote.

2.5 Nadharia ya Mawasiliano

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mawasiliano iliyoshika kasi nakupanuka nchini Uingereza katika miaka ya 1970 Paul M., Musau, Leonard M., Chacha (2001) lengo kuu ya nadharia hii ni kukuza uwezo wa kuwasiliana lakini siyo kukuza ujuzi wa miundo au vipengele vya lugha tu. Inakusudiwa kukidhi matakwa ya wale wanaojifunza lugha ya pili katika kuwasiliana. Mawasiliano yanahusu mambo mengi.

kama vile kusababisha mambo fulani yafanyike, kuboresha mahusiano kati ya watu na kuonyesha hisia za watu na ubunifu wao.

Kadhalika nadharia hii ilikusudiwa kuimalisha mbinu za ufundishaji ambazo zinasisitiza uhusiano uliopo kati ya miundo ya Lugha na mawasiliano hivyo nadharia hii imemsaidia sana mtafiti kumwongoza na kusimamia misingi na mipaka ya nadharia hii. Maana ya miundo husisitizwa kwani lengo kubwa la nadharia ni mawasiliano. Kwa mujibu wa nadharia hii, madhumuni makuu ya Lugha ni kuwasiliana, kwani lugha ni mfumo wa kueleza maana.

Vipashio vya Lugha sio vile vya Sarufi na kimuundo tu, lakini pia vile vya kimawasiliano. Matamshi yanayotolewa na Watu wengi katika mazungumzo ndio lengo kuu. Lengo sio matamshi yanayofanana na yale ya wazawa wa Lugha. Mazingira hupewa nafasi muhimu katika suala zima la ufundishaji, kwa mfano maneno mapya au muundo fulani ya kisarufi huwekwa katika muktadha wa mawasiliano. Kusoma na kuandika kunaweza kuanza katika siku za mwanzo na kuendelea ikiwa ni muhimu. Nadharia ya mawasiliano ilipendekeza ufundishaji ambao unatumia shughuli zinazoendeleza mawasiliano. Hii ni kwa sababu wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa ujifunzaji wa Lugha huendelezwa na vitendo au shughuli zinaelekeza mawasiliano.

2.6 Hitimisho

Katika sura hii tulizungumzia kuhusu utangulizi, kwa kueleza maana ya mapitio ya kazia tangulizi, pia tumeonesha mapitio mbalimbali ya kazi tangulizi, pengo la utafiti, kiunzi cha nadharia na nadharia ya mawasiliano.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data. Kothari (2008) anaeleza kwamba utafiti wowote ule wa kitaaluma ni lazima ufanywe kwa kuongozwa na mbinu mbalimbali za utafiti ili uweze kutoa matokeo yasiyo na shaka ndani yake kwa msingi huo basi, zifuatazo ni mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika kukusanya data za utafiti huu kama zinavyoelezwa hapa chini:-

3.2 Mbinu za Ukusanyaji Data

Kuhusu utekelezaji wa kuzikusanya data kwa njia shirikishi. Ukusanyaji wa data ulifanyika katika Mkoa wa Mara Wilaya ya Butiama. Utafiti ulikusanya data kutoka katika Taasisi mbili kutoka Kata ya Bwasi na Kata ya Makojo. Utafiti huu ulifanyika katika Shule ya Msingi Chimati A na Bulinga A. Mtafiti aliwashirikisha Waalimu, Wanafunzi na Wataalamu (Wazazi) wa lugha ya Kijita.

Utafiti huu ulitumia mbinu ya hojaji na dodoso katika kukusanya data. Utafiti huu ulitumia mbinu ya dodoso kwa sababu hukusanya data kwa watafutiwa wengi kwa muda mfupi. Mbinu ya hojaji ilitumika katika makundi yote, ili kupata taarifa zilizo sahihi toka makundi yote tofauti. Yaani Walimu, Wanafunzi na Wataalamu (Wazazi). Data ya awali ilipatikana kutoka katika maktaba kwa kusoma Vitabu na makala zilizohusiana na athari za Lugha na jinsi zilivyoathiri Lugha ya Kiswahili, utafiti pia ulipendekeza mbinu za kutumia ili kuwasaidia Watu hao. Mbinu hizo za ukusanyaji wa data zilisaidia kukusanya taarifa za kutosha katika utafiti.

3.3 Data ya Awali/Upili

Mtafiti alisoma kazi tangulizi katika maktaba mbalimbali nchini hususani maktaba ya mkoa wa Tabora, Maktaba ya Mkoa wa Mara na Maktaba ya Chuo kikuu Huria cha Dar es saalam Tanzania, kutoka katika Vitabu na makala mbalimbali wakati wa kukusanya data zake.

3.4 Dodoso

Mtafiti aliandaa dodoso za aina tatu. Aina ya kwanza ya dodoso ilikuwa na maswali 8 na jumla ya Walimu walikuwa Shule ya Msingi Chimati A walikuwa 8 na Shule ya Msingi Bulinga A walikuwa ni Walimu 6. Lengo la kuhusisha Walimu ilikuwa kuweza kuelewa jinsi wanafunzi wa lugha ya kijita wanavyojifunza lugha ya Kiswahili. Dodoso la pili liliandaliwa kwa ajili ya wanafunzi likiwa na jumla ya maswali 7. wanafunzi wa Shule ya Msingi Chimati A walikuwa wanafunzi wa darasa la saba, sita, na darasa la tano. Jumla walikuwa ni wanafunzi 18. Shule ya Msingi Bulinga A

walikuwa wanafunzi wa darasa la saba 22, darasa la sita 10, na darasa la tano 15. Jumla walikuwa ni wanafunzi 37. Dodoso la tatu lilikuwa ni la wataalamu (Wazazi) Kijiji cha Chimati walikuwa wataalamu (Wazazi) 12 na Kijiji cha Bugunda walikuwa ni 15. Kulikuwa na jumla ya maswali 7 katika dodoso la utafiti.

3.5 Hojaji

Kwa mujibu wa Buliba (mwaka haujatajwa UK 90), hojaji ni seti ya maswali yaliyoandikwa au kauli zinazohusiana na suala linalotafitiwa ambalo mtafiti hutoa kwa wasailiwa kwa minajili ya kuibua habari, majibu, maoni, mitazamo na mikabala mahususi kuhusu mada ya utafiti. Hivyo njia hii imetumia maswali yaliyoandikwa yanayoweza kuwa na majibu mafupi au marefu kutegemeana na taarifa inayohitajika. Maswali yanaweza kuwa Maswali funge au maswali wazi. Mbogo na wenzake (2012:97) katika kitabu chao cha Research Methodology cha Mwaka 2012, wanasema kuwa maswali yafaa kuwa mafupi yasiyozidi dakika 20.

Mtafiti aliandaa swali moja tofauti tofaouti la hojaji katika makundi yote matatu ambayo yalikuwa ni walimu jumla 14 kwa shule zote mbili, wanafunzi wa shule ya Msingi Chimati A walikuwa 18 na shule ya Msingi Bulinga A walikuwa wanafunzi 37 na wataalamu (Wazazi) Kijiji cha Chimati walikuwa 12 na Kijiji cha Bugunda walikuwa 15. Mtafiti alitumia mbinu hii kuweza kupata taarifa alizokuwa amekusudia kuzipata katika utafiti wake. Kwa mujibu wa Kothari kuna maswali ya Hojaji aina mbili. Aina ya kwanza ni maswali funge na aina ya pili ni maswali ya wazi. Mtafiti alitumia maswali ya wazi kwa makundi yote matatu ya watafitiwa ili kuwapa nafasi ya kujieleza kulingana na maswali ya mtafiti aliyoandaa kwavile yanahitaji kusikia athari za matamshi ya mwanafunzi alivyoathiriwa na hiyo lugha mama. Kwa kufanya hivyo

kulimsaidia mtafiti kupata taarifa za utafiti alizokuwa amekusudia kuzipata katika utafiti wake. Mbinu ya Hojaji ina faida zifuatazo:

- i. Inafaa kukusanya data katika kundi kubwa
- ii. Data zake huchanganuliwa kwa urahisi
- iii. Ina usaili wa majibu
- iv. Inatumia muda mfupi zaidi hasa maswali ya papo kwa papo

3.5.1 Mahojiano/Usaili

Kwa mujibu wa Kothali (kesha tajwa) mbinu hii ina husu kuwauliza maswali wasailiwa. Yaweza kuwa majibizano ya ana kwa ana au simu kati ya watu wawili au kundi la watu kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti. Mahojiano yanaweza kuwa ya namna zifuatazo:

- (i) Mahojiano ya ana kwa ana baina ya watu wawili.
- (ii) Mahojiano baina ya mtu na kikundi cha watu na kikundi kingine.
- (iii) Mahojiano ya simu.

Katika utafiti huu Mtafiti ametumia mahojiano ya ana kwa ana baina yake na mtafitiwa mmoja mmoja. Mtafiti alikuwa na mwongozo wa maswali ambayo aliwauliza Watafitiwa maswali yalijibiwa kwa njia ya mdomo na Mtafiti akarekodi majibu kwa ajili ya kumbukumbu aidha Mtafiti alikuwa na daftari ambamo alinukuu maswali ya usaili pamoja na majibu yaliyotolewa na Watafitiwa ili kuepuka upotevu wa kumbukumbu endapo kinasa sauti kitapatwa na hitilafu.

Faida kuu za mbinu hii kulingana na Babbie (2005) ni kwamba:

- (i) Kupata ufafanuzi wa majibu yanayotolewa na watafitiwa kwa kuwa majibu hutolewa ana kwa ana.
- (ii) Inampa Mtafiti uwezo wa kuuliza maswali ya ziada hivyo kuondoa utata wa maana katika majibu yaliyotolewa jambo ambalo si rahisi kwa njia ya hojaji.
- (iii) Inampa Mtafitiwa uwezo wa kuuliza maswali ya ziada hivyo kutoa majibu yaliyosahihi zaidi jambo ambalo si rahisi kwa njia ya hojaji. Njia hii humpa uhakika Mtafiti kuwa walengwa wake ndio wamejibu maswali yake jambo ambalo si rahisi kwa njia ya hojaji.

Mtafiti alitumia njia hii katika makundi ya wanafunzi walikuwa wanne (4), walimu walikuwa wa (3) na wataalamu (Wazazi) walikuwa wawili. Mtafiti alitumia aina hizo zote tatu za utafiti ili aweza kupata taarifa za kutosha na ambazo ziko sahihi kulingana na alivyokusudia katika utafiti wake wakati wa kukusanya data zake. Umuhimu wa kila mbinu aliotumia mtafiti ni kuwa ililenga kupata taarifa kwa kila kundi ili kulinganisha utafiti wake kwa kila njia aliyotumia ili kulinganisha taarifa za kila mbinu na kila kundi lililohusika katika utafiti wa mtafiti. Katika utafiti huu mtafiti aliamua kutumia madarasa ya tano, sita na saba kwa sababu ndio madarasa ambayo kuzungumza kiswahili fasaha kwa kuzingatia eneo husika lililokuwa linafanyiwa utafiti ambalo ni eneo la Kijijini. Hivyo madarasa hayo yanaweza kutoa muelekeo mzuri wa utafiti.

3.6 Data za Msingi

Benard (2012) data za msingi ni zile anazozipata mtafiti moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa, utafiti hutumia mbinu kama dodoso, hojaji na mahojiano ya makundi

katika kukusanya data (ty). Mtafiti ametumia data za msingi kwa kiasi kikubwa katika utafiti wake. Taarafa hizo zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na athari za Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili. Data za msingi zilisaidia kukusanya na kupata taarifa sahihi kuhusiana na mada, kama tujuavyo taarifa hizi hazipatikani mpaka mtafiti awatembelee watafitiwa ili aweze kupata taarifa kuhusiana na kile alichopanga kukitafiti. Hivyo mtafiti aliwatembelea watafitiwa ili aweze kupata taarifa kuhusiana na kile alichopanga kukitafiti. Hivyo mtafiti aliwatembelea watafitiwa na kupata taarifa alizotegemea kuzipata kutokana na mada yake.

3.7 Sampuli na Njia za Usampulishaji

Kundi Lengwa

Ni kundi ambalo mtafiti amekusudia kukusanya taarifa za kiutafiti kwenye hilo kundi ambalo linakuwa ni kundi dogo alilokusudia kufanyia utafiti wake. Ingule (1988) anasema sampuli ni kundi dogo ambalo ni kiwakilishi cha kundi kubwa. Ni wazi kuwa huwezi kukutana na watu wote waliokatika eneo la utafiti, hivyo ni lazima kuchagua watu wachache kutoka kundi lengwa ili kupata watu wachache watakaofanyiwa utafiti ambao watawakilisha kundi kubwa. Utafiti ulihusisha Walimu shule ya Msingi Chimati A walikuwa 8 wanafunzi walikuwa darasa la saba, sita na darasa la tano. Jumla 18, na waalamu (Wazazi) walikuwa 12 kwa upande wa shule ya Msingi Bulinga A walimu walikuwa sita, wanafunzi darasa la saba 22, darasa sita walikuwa 10 na darasa la tano 15 na waalamu (Wazazi) katika Kijiji cha Bugunda walikuwa 15. Sababu za kuchagua kundi hili ni kutokana na kwamba ni kundi ambalo bado halina umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa kutosha na hivyo linaathiriwa zaidi na uhamishaji

wa mazoea ya Lugha ya kwanza (L1) kwenda Lugha ya pili (L2) yaani maneno ya Lugha ya Kijita huhamishwa kwenda Lugha ya pili ya Kiswahili.

3.8 Uteuzi wa Sampuli

Utaratibu wa kuwapata watafitiwa kutoka kwenye kundi lengwa hujulikana kama usampulishaji. Kuna njia nyingi za kupata Sampuli, mbinu ya kukusudia (isiyo nasibu), mbinu ya bahatishi (usampulishaji nasibu), mbinu ya madhumuni maalumu na kadharika kutegemeana na uraisi wa kupata taarifa inayohitajika. Kwa mujibu wa Ingule (1988), Uchaguzi usio wa kukusudia ni ule ambao mtafitiwa huteuliwa kutokana na vigezo alivyonavyo au taarifa aliyonayo kuhusu utafiti unaofanyika.

Katika utafiti huu, mtafiti ametumia njia ya kukusudia (isiyo nasibu) na mbinu bahatishi (usampulishaji bahatishi) mtafiti alitumia mbinu hizo ili kufikia malengo yake aliyokusudia. Kuona athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili ilivyo na mgawanyiko kwa watu tafauti na mfuatano wa maneno katika lugha. Kothali (2004) anasema kuwa mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti.

3.9 Mkabala wa Utafiti

Kwa mujibu wa Buliba data huweza kuchanganuliwa kwa kutumia mikabara mikuu miwili. Mikabala hiyo ni ule wa kiidadi na wakimaelezo (au usiyo wa kiidadi) Mkabala wa kiidadi hutumiwa zaidi kurekodi taarifa na kuchanganuliwa kwa kutumia takwimu, naye Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi na mbinu ya kuchunguza data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia

maelezo. Katika utafiti huu mtafiti atatumia mkabala wa kimaelezo kwa mujibu wa Buliba na wenzake (kesha tajwa) asilimia kubwa ya tafiti zinazo husu Lugha, ni za kimaelezo wanasema aina hii ya utafiti huwa haina mambo mengi changamani, hii ni kwa sababu utafiti hulenga jinsi mambo yalivyo pasipo kubadili.

3.9.1 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti vilivyotumika katiak utafiti huu ni pamoja na Karatasi za rimu, Karamu, Kompyuta mpakato, Kinasa sauti, Daftari la maswali na majibu ya mahojiano, Penseli, Dodoso, Kikokotoa, Mkoba, Marejeo, Shajara na kinyoyi.

3.9.2 Eneo laUtafiti

Data za utafiti huu kuhusu athari ya Lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili zilikusanywa Vijijini katika Mkoa wa Mara, Wilaya ya Butiama na Tarafa ya Nyanja ambapo katika eneo hili ndiko waliko wazungumzaji wa Lugha ya Kijita asili.

3.10 Hitimisho

Sehemu hii ilifafanua utafiti ulivyofanyika kwa undani, sehemu ya kwanza inayohusu eneo la utafiti, mbinu za ukusanyaji data, sehemu ya pili inayohusu kundi lengwa, sehemu ya tatu inayohusu sampuli na utaratibu wa usampulishaji, sehemu ya nne inayohusu na sehemu ya tano inaeleza kuhusu vifaa vilivyotumika katika utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii ilihusisha taarifa zilizokusanywa wakati wa utafiti huu katika vijiji vya Chimati na Bugunda ambapo pia ilihusisha shule za Msingi Bulinga A na Chimati A, Walimu wa shule hizo pamoja na wataalamu (Wazazi) walugha ya kijita hii ni sehemu iliyojishughulisha na uwasilishaji wa data, na uchambuzi wa data. Makundi matatu yalikusishwa katika taarifa hizi makundi hayo ni walimu, wanafunzi pamoja na wataalamu (Wazazi). Utafiti huu ulifanikiwa kufikia malengo yake mahsusi wakati wa ukusanyaji data zilizohusiana na mada ya utafiti kwa kuhusisha jumla ya watafitiwa 96 idadi ya kila kundi ilikuwa kama ifuatavyo: Walimu katika Shule ya Msingi Chimati A walikuwa 8 wanafunzi walikuwa darasa la saba, la sita na la tano jumla 18 na wataalamu (wazazi) walikuwa 12 kwa upande wa shule ya Msingi Bulinga A walimu walikuwa 6, wanafunzi walikuwa darasa la saba 22, darasa la sita walikuwa 10 na darasa la tano walikuwa 5 na wataalamu (wazazi) katika kijiji cha Bugunda walikuwa 15. Hivyo jumla walimu walikuwa 14, wanafunzi walikuwa 55 na Wataalamu (wazazi) walikuwa 27.

4.1.1 Maswali ya Utafiti Yaliyoulizwa

4.2 Athari ya Lugha ya Kijita katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili

Lugha mama ina athari nyingi wakati wa kujifunza lugha nyingine. Mtu anayejifunza lugha hukumbana na vikwazo na matatizo mbalimbali yanayo weza kumzuia wakati wa kujifunza na kuwasiliana kwa mawasiliano yanapokuwa hayapo katika upande mmoja basi huonyesha kuna udhaifu katika mawasiliano kama data zifuatazo zinavyochanganuliwa.

4.2.1 Mwanafunzi Kutomuelewa Mwalimu Wakati wa Kufundishwa

Mawasiliano ni kitu muhimu kwa watu katika kuwasiliana ndani ya jamii. Athari ya lugha ya Kijita husababisha kukwamisha lengo la mawasiliano. Chacha (2011) anasema kuwa lengo kuu la nadharia ya mawasiliano ni kukuza uwezo wa kuwasiliana. Chanzo cha data hizi ni kutokana na maswali ya dodoso yaliyoulizwa kwa makundi yote matatu ya watafitiwa yaani Walimu, Wanafunzi na Wataalamu (Wazazi) kuhusu Wanafunzi kuwasiliana na wazazi wao wanapokuwa nyumbani. Waliojibu dodoso hili walisema hutumia lugha ya Kijita. Idadi ya Walimu, Wanafunzi na Wataalamu (Wazazi) ilikuwa 96 kati ya hao waliojibu ni 88 ambayo ni sawa na 92%

Jedwali Na. 4.1: Idadi ya Watafitiwa Kutomwelewa Mwalimu Wakati wa

Kufundishwa kutokana na athari ya Kijita

Idadi ya Watafitiwa	Ambao hawakusema	Waliokubaliana na hoja
96	8	88

Rocha (2011) anaeleza kuwa wabantu wengi wameathiriwa na lugha mama. Watafitiwa wanafunzi walioulizwa swali la dodoso kuhusu lugha mama ambalo

liliuliza ipi ni lugha mama kati ya lugha ya Kijita na lugha ya Kiswahili? Watafitiwa wote walijibu ni lugha ya Kijita.

Utafiti uligundua kwamba Mwalimu anaposhindwa kupokea au kufikisha dhumuni alilolenga kwa wanafunzi wake huwa inasababisha kutokuelewana baina ya Mwalimu na Mwanafunzi wakati wa ujifunzaji, hii hutokana na athari alizonazo Mwalimu au Mwanafunzi mwenyewe. Wanafunzi walio wengi wa kijita huwa wameathiriwa na lugha yao mama kutokana na matumizi ya lugha hiyo kwa kipindi kirefu.

4.2.2 Kuongeza Viambishi Visivyohitajika

Wanafunzi wa lugha ya Kiswahili walioathiriwa na lugha ya kijita huongeza viambishi mahali pasipo hitajika hufanya hivyo wakati wa kuongea lugha ya Kiswahili nia yao ni kukidhi mazungumzo ya muda huo. Kiini cha data hii ni kulingana na watafitiwa Walimu, Wanafunzi na Wataalamu (wazazi) waliojibu maswali ya dodoso yaliyouliza kiisimu ni maneno gani ya lahaja ya kijita yanayoathiri matamshi ya lugha ya kiswahili na orodhesha maneno matano ambayo yanaonyesha athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili sanifu.

Majibu yaliyotolewa na watafitiwa katika makundi yote matatu yanaonyesha kuwa Wajita wanaongeza maneno (viambishi) mwishoni mwa mzizi wa neno ambavyo sivyo vya lazima katika lugha tofauti kutokana na lugha ya kiswahili sanifu. Mifano ya baadhi ya vitamkwa vinavyoongezwa kama ilivyooneshwa na watafitiwa ni hii ifuatayo kutoka katika lugha ya kijita maneno yanayoonesha umahali – vitenzi katika kijita kuna vitamkwa au maneno madogo madogo yanayoonesha mahali, yaani, - ko,

- mo, - yo, - wo, ambayo hutokea mara tu ya kutamka vitenzi. Tunapoandika maneno haya pamoja na vitenzi, basi tuyatenganishe na vitenzi kwa kutumia kistali (-) kama ilivyo katika nomino. Kwa mfano:

1. Chije – yo.
2. Gega – mo.
3. Itwikira – mo.
4. Kaayamba – mo.
5. Riinya – ko.
6. Yaanikira – ko.

Hivyo Mwanafunzi wa Kijita atahamisha viambishi hivyo vya Kijita na kuvipeleka katika lugha ya Kiswahili kama inavyoonesha kutoka kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 4.2: Kuongeza Viambishi Visivyohitajika

Maneno ya kiswahili	Vitamkwa vinavyoongezwa na wazungumzaji wa lugha ya kijita
Peleka	Peleka – ko
Chukuwa	Chukua – mo
Beba	Beba - mo
Tucheze	Tucheze – ko
Tazama	Tazama – po
Sema	Sema - po
Nenda	Nenda – po
Toka	Toka – ko
Cheza	Cheza – po

Chungulia	Chungulia – po
Sikia	Sikia – po
Kariri	Kariri – ko
Soma	Soma – po
Imba	Imba – ko
Nipe	Nipe – ko
Tutaonana	Tutaonana – po
Songa	Songa – ko
Cheka	Cheka – ko
Lima	Lima – ko

Wazungumzaji wa Kiswahili Sanifu wanaposikia utamkaji wa maneno ya Kiswahili Sanifu kwa namna hiyo hutambua wazi kuwa, Mwanafunzi hana umilisi katika lugha ya Kiswahili Sanifu ni rahisi sana kwa anayefahamu kuelewa na kubashiri kuwa Mwanafunzi huyu ni mtu aliyeathiriwa na lugha ya Kijita. Mtaalamu wa Kiswahili hugundua kwa sababu, huwa tayari anajua sauti za lugha ya kiswahili zinatamkwaje na mahali pa kutamkia utafauti unaonekana pale Mwanafunzi anapotamka sauti za Kiswahili maana atatumia matamshi na lafudhi ya lugha ya kijita. Mwanafunzi wa lugha ya Kijita hutumia nguvu ya kukaza maneno sana wakati wa kutamka maneno kwa hali hiyo wakati wa kuzungumza kiswahili hutumia hali na nguvu ile ile ndiyo sababu wanaongeza maneno kwa kuweka mkazo hata pale pasipo stahili kufanya hivyo katika utamkaji wa maneno. Utofauti huu huleta mabadiliko katika matamshi ya lugha ya Kiswahili kutokana na athari kubwa ya lugha ya kijita kwa Mwanafunzi. Yule anayeweza kufahamu utafauti huu ni lazima awe anafahamu bayana lugha ya

Kiswahili Sanifu Kihore (2009) alieleza kuwa utaratibu wa mpangilio wa viambishi huwa katika mfuatano unaotupatia silabi zinazokubalika katika lugha kama ifuatavyo katika mifano hii:-

Analima a – na – lim – a

- a – kiambishi awali nafsi ya tatu umoja
- na – kiambishi cha njeo ya wakati uliopo
- lim – kiini (Mzizi wa neno)
- a – kiambishi tamati.

Anacheza a – na – chez – a

- a – ni kiambishi awali nafsi ya tatu umoja
- na – kiambishi cha njeo wakati uliopo
- chez – kiini (Mzizi wa neno)
- a – kiambishi tamati.

Katika mifano hiyo hapo juu kila kiambishi katika neno kina maana kulingana na muktadha wa matumizi yake, Idarus (2005) anaonyesha athari zinazojitokeza katika lugha ya kiswahili baada ya mwanafunzi kuathiriwa na lugha ya Kijita. Idarus anasema athari hizo ni kama makosa ya muundo wa sentensi, makosa katika matamshi, kuongeza vitamkwa vya maneno, sauti pasipo hitajika, Msamiati wa lugha. Hii ni dhahiri kuwa lugha ya Kijita imemuathiri mwanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulionyesha kuwa wanafunazi walioathiriwa na lugha ya Kijita wengi wao ni katika maeneo ya majita A na B. Mambo mengi sana mtafiti alibaini kwa watafitiwa kuhusu kuathiriwa kwao.

4.2.3 Athari katika Matamshi

Taarifa hii inatokana na watafitiwa walimu na wanafunzi waliojibu swali la hojaji lililouliza je, ni athari zipi za kimatamshi zinazojitokeza kwa Wanafunzi wa Kijita wanapojifunza lugha ya kiswahili?

Jedwali Na. 4.3: Idadi ya Watafitiwa wa Hojaji uhusu Athari katika Matamshi

Idadi ya watafitiwa	ambao hawakusema	Waliosema
69	4	65

Kutokana na jedwali hilo ni dhahiri kuwa Wanafunzi wengi wa Kijita wameathiriwa na matamshi katika utamkaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili. Hii inatokana na kuhamisha maneno ya Kijita na kuyapeleka katika lugha ya Kiswahili kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo juu matamshi ni athari moja wapo kubwa ambayo inayokwamisha mawasiliano kati ya wale wanaopashana habari maana matamshi ni msingi mkubwa wa mawasiliano unaposhindwa kutamka maneno vizuri huweza kuathiri mawasiliano baina ya watu, Mwanafunzi anaposhindwa kutamka maneno inavyotakiwa hukwamisha mawasiliano kutofikishwa kama ilivyokusudiwa na Msikilizaji.

Leonard (2011) anahusisha umuhimu wa mawasiliano ni kukuza uwezo wa kuwasiliana. Matamshi ni msingi muhimu sana katika mawasiliano, hii ina maana kuwa unapojifunza lugha matamshi lazima ujifunze ili katika mawasiliano pasiwepo na kutokuelewana kwa pande mbili zinazohusika. Kuna baadhi ya Mifano kutoka kwa wanafunzi wa lugha ya kijita jinsi ambavyo wanavyoathiriwa na wanavyotamka

maneno hayo kwa lugha yao ya Kijita kisha kuhamisha matamshi na lafudhi ya maneno hayo katika lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na. 4.4: Kuhusu Athari za Matamshi

Kijita	Kiswahili Sanifu
Muti	Mti
Jaakariya	Zakaria
Maryamu	Mariamamu
Taabhu	Taabu
Mutihani	Mtihani
Simooni	Simoni
Yeesu	Yesu
Gaabhuryeri	Gaburieli
Muto	Mto
Umbwa	Mbwa
Yine	Nne
Adaamu	Adam
Jaabheeti	Elizabethi
Ayupo	Hayupo
Apana	Hapana
Kura	Kula
Chikombe	Kikombe
Mutu	Mtu
Jaabhuroni	Zabroni

Binadamu anautaratibu utumikao katika kutoa maneno ya matamshi. Neno matamshi kwa watu wengi walilinganisha na maneno mabaya. Lakini katika lugha huwa kuna maana ya utoaji wa maneno husika. Yule (2010) anasema kuwa matamshi ni utamkaji wa sauti za binadamu kwa kuzingatia Mukadha wa mazungumzo. Nkwera (1979) anasema kuwa nguzo kuu ya mawasiliano mazuri ni utoaji wa matamshi yanayoeleweka kwa msikilizaji wake. Naye Lucius (1978) anasema kwamba, kanuni na Misingi ya lugha ndizo zinazotawala lugha za watu wote kwa ujumla. Kila lugha inautaratibu na Misingi maalumu inazozihusu lugha fulani tu, ambayo huifanya iwe tofauti na lugha nyingine. Lugha yetu ya Kiswahili pia ina Misingi na Kanuni hizo maalumu.

4.2.4 Msamiati

Matumizi ya lugha zaidi ya moja katika jamii husababisha mwingiliano katika Msamiati wa lugha katika jamii husika. Data hii chanzo chake ni kutokana na Watafitiwa Wanafunzi waliojibu dodoso lililohoji kuwa, Je matumizi ya lugha zaidi ya moja katika jamii husababisha mwingiliano katika Msamiati wa lugha katika jamii husika?

Jedwali Na. 4.5: Idadi ya Watafitiwa Kuhusu Mwingiliano katika Msamiati wa Lugha

Idadi ya Watafitiwa	Ndiyo	Hapana
55	43	12

Kutokana na data iliyopo hapo juu kwenye jedwali Watafitiwa wengi wameonesha kuwa kuna tatizo la Msamiati wa lugha kuwa na mwingiliano kutoka lugha mama ya

Kijita kwenda lugha ya kiswahili. Hivyo panakuwepo na mwingiliano wa Msamiati kutoka lugha moja kwenda Msamiati wa lugha nyingine tofauti.

Rugatiri (2011) anaeleza kuwa Msamiati ni Nyanja muhimu katika kuwasiliana, hii ina maana kuwa Msamiati ndio unaonogesha Mawasiliano. Uteuzi wa Msamiati kwa kuangalia utumizi wake kuboresha mawasiliano baina ya wazungumzaji, kama nadharia ya Mawasiliano ilivyoelezwa na Mwasisi, Musau (2011) kuwa mawasiliano huboresha mahusiano kati ya watu. Hii inaweza kuboreshwa endapo matumizi ya Msamiati yatazingatiwa na Mazungumzo. Msamiati ni istilahi iliyo muhimu sana katika kuwasiliana, Mzungumzaji anatakiwa awe makini katika uteuzi wa Msamiati unaoendana na Mukadha wa Mazungumzo.

4.3 Ni Sababu Zipi Zinazochangia Kuwaathiri Wanafunzi wa Kijita Wakati wa Kujifunza Lugha ya Kiswahili

Utafiti huu ulionyesha kuwa wanafunzi wawapo shuleni wanatumia lugha ya kijita zaidi katika mawasiliano ya wao kwa wao kuliko lugha ya kiswahili sanifu. Taarifa hii imetokana na data ya watafitiwa walimu waliojibu dodoso iliyouliza. Je, wanafunzi wa shuleni kwako wanazungumza lugha ya Kiswahili Sanifu? Watafitiwa waliojibu swali hili wamesema hapana kwa sababu wanafunzi wameathiriwa na lugha mama hii inadhihirishwa na taarifa kutoka kwa watafitiwa walimu kama ilivyo kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 4.6: Idadi ya Watafitiwa wa Athari ya Lugha ya Kijita katika**Kujifunza Lugha ya Kiswahili**

Idadi ya Walimu	Kijita	Kiswahili
14	12	2

Watafitiwa Walimu 12 ambao ni sawa na asilimia 86 walijibu kwamba, lugha ya kijita imewaathiri wanafunzi katika mawasiliano wanapokuwa shuleni.

Sababu ni kwamba wanapokuwa shuleni wanapowasiliana wao kwa wao wanatumia lugha ya kijita kwa vile ni lugha mama kwao. Hivyo pana haja ya uongozi wa shule kuwa na mpango mkakati mzuri wa jinsi ya utumiaji wa lugha ya kiswahili kwa hao wanafunzi wanapokuwa katika mazingira ya shuleni, kama vile kuwa na uwanzishwaji wa vikundi au vilabu vya masomo vitakavyosaidia kuinua hali ya uzungumzwaji wa lugha ya kiswahili sanifu kwa kila shule. Mekacha (2011) anasema lugha moja huathiriwa kulingana na Mukadha wa matumizi yake. Lugha ya Kiswahili hutumiwa katika shughuli za kiserikali kama vile maofisini, shuleni (kwenye Taasisi) katika mikusanyiko ya watu wengi wa kabila tofauti ndipo kiswahii hutumika ili kuwakutanisha. Watu wengi wanapokuwa nyumbani kwa kiasi kikubwa hutumia lugha zao za asili.

4.4 Lugha Nyingi katika Jamii

Kutokana na utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa matumizi ya lugha zaidi ya moja katika jamii yanaleta athari katika lugha. Hii ni kutokana na data kwa watafitiwa Wanafunzi waliojibu dodoso lililouliza je, unapotumia lugha zaidi ya moja, Mfano kijita, kiswahili au kiingereza kuna athari zozote zinazojitokeza?

Jedwali Na. 4.7: Idadi ya Watafitiwa Waliojibu Kuhusu Lugha nyingi katika jamii

Idadi ya Watafitiwa	Ndiyo	Hapana	Hakuna jibu
55	46	7	2

Jumla ya Watafitiwa 46 ambao ni sawa na asilimia 84 walisema ndiyo sababu kuu ni kwamba lugha ya kwanza ambayo mtoto hujifunza kwa mara ya kwanza humjengea mizizi na misingi katika Nyanja zote za mfumo wa sauti. Anapoanza kujifunza lugha nyingine, huwepo na athari ambazo hujitokeza katika ujifunzaji wa lugha nyingine. Nadharia ya Mawasiliano. Leonard (2001) kama waasisi walivyosema kuwa lengo kuu ni kukuza uwezo wa kuwasiliana. Kuwa na lugha zaidi ya lugha moja husababisha lugha moja kuathiriwa kama kiswahili kilivyoathiriwa na lugha ya kijita. Lugha ya Kiswahili hutumiwa hasa katika shughuli za kijamii zaidi kama vile ofisini, shuleni, sehemu za kazi, biashara na sehemu ambazo kuna makabila mengi ndipo kiswahili hutumika ili kuwakutanisha. Mekacha (2011), anasema lugha moja huathiriwa kutokana na Mukadha wa matumizi ya lugha hiyo.

4.4.1 Mukadha

Kutokana na utafiti uliofanyika inaonesha kwamba Mazingira ni sababu moja wapo inayowaathiri katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Data hii inatokana na watafitiwa Walimu waliojibu swali la dodoso lililokuwa linauliza kuwa je, Mazingira yanaweza kuwa ni sababu moja wapo ya kuwaathiri wanafunazi wa kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili?

Jedwali Na. 4.8: Idadi ya Watafitiwa Waliojibu Dodoso Kuhusu Mukstadha

Idadi ya Walimu	Ndiyo	Hapana
14	14	0

Kama inavyoonesha kutoka kwenye jedwali hapo juu. Utafiti unaonesha kwamba Watafitiwa 14 ambao ni sawa na asilimia 100 wamesema mazingira ni moja wapo ya sababu ya kuwaathiri wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Nadharia ya mawasiliano inalenga kukidhi matakwa ya wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili katika kuwasiliana. Mwanafunzi aliyezaliwa katika Jamii fulani, ambapo jamii hiyo hutumia lugha ya jamii wakati mwingi inakuwa vigumu sana kwa mwanafunzi huyu kuwa mzungumzaji mzuri wa lugha ya pili kwa sababu lugha ya kwanza huitumia kwa muda mwingi katika mawasiliano. Mazingira ya vijiji vya Majita wanafunzi wengi huwa wameathiriwa na lugha mama, maana matumizi ya lugha ya kiswahili ni kidogo sana, Mawasiliano mengi hufanywa kwa kutumia lugha mama. Mekacha (2011), anasema lugha moja huathiriwa kutokana na Mukstadha wa matumizi yake, moja wapo ya athari inayochangia ni Mazingira yanayojumuisha nyumbani pamoja na Jamii yake inayomzunguka. Vilevile Paul (2001), anasema Mazingira hupewa nafasi muhimu katika ufundishaji, hivyo Mwanafunzi anapojifunza lugha fulani, Mazingira ni muhimu kuangaliwa.

Wazazi wanapotumia lugha ya kijita kwa muda wote nyumbani, hutoa picha ya kuwaathiri watoto wao wakati wanapojifunza lugha nyingine. Chanzo cha data hii ni kwa Watafitiwa Walimu, Wanafunzi na Wataalamu (Wazazi) waliojibu swali la

dodoso lililokuwa linauliza je, Wanafunzi wanapokuwa nyumbani wanatumia lugha ipi katika kuwasiliana na Wazazi wao?

Jedwali Na. 4.9: Matumizi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi

Wanapokuwa Nyumbani

Idadi ya Watafitiwa	Lugha ya Kijita	Lugha ya Kiswahili	Majibu yote ni sahihi
96	85	6	5

Kutokana na data iliyotolewa hapo juu kwenye jedwali Watafitiwa 85 sawa na asiliamia 89 walisema Wanafunzi wanawasiliana na Wazazi wao kwa lugha ya Kijita. Nadharia ya mawasiliano hukusudia pia kuboresha mahusiano baina ya watu na kuonesha hisia za watu. Rocha (2011) lugha mama na lugha ya pili, kwa watanzania wengi lugha mama ndiyo lugha ya kwanza kujifunza maana huzaliwa na kuikuta katika Jamii yake na lugha ya kiswahili huwa ni lugha yake ya pili kwa mujibu wa Watanzania wenyewe. Si watanzania wote kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili wengine ni kama lugha yao mama maana huzaliwa na kuikuta katika mazingira yao.

Wazazi wengi walio katika Mazingira ya vijijini hawazungumzi lugha ya Kiswahili na huzungumza lugha mama kwa muda mwingi sana na watoto wao kwa sababu tangu kuzaliwa na jinsi anavyoendelea kukua katika Mazingira yanayomzunguka watu wote sehemu kubwa wanaongea lugha mama hivyo wanajenga mazoea hayo ya kutoongea Kiswahili sanifu hii ni kutokana na athari ya lugha mama kuitumia muda mwingi.

4.4.2 Tatizo la Kiswahili Shuleni

Chanzo cha data hii ni Watafitiwa Wanafunzi waliojibu dodoso lililouliza je, ni sababu gani zinazochangia Wanafunzi wa kijita katika kushindwa kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu wawapo shuleni?

Jedwali Na. 4.10: Data ya Watafitiwa Wanafunzi Kuhusu Tatizo la Kutumia

Lugha ya Kiswahili Shuleni

Idadi ya Wanafunzi	Kiswahili	Kijita
55	5	50

Jumla ya watafitiwa 50 ambao ni sawa na 91% walisema lugha mama ya kijita ndio inawafanya wanafunzi kuwa na tatizo la kuzungumza lugha ya Kiswahili Sanifu wawapo shuleni.

Lugha ya Kijita kwa Wanafunzi wa Kijita kwao ni lugha mama, hivyo wanapokuwa katika Mazingira ya shuleni bado wanaendelea kutumia lugha hiyo mama ili kufanikisha Mawasiliano ya wao kwa wao.

4.5 Jinsi ya Kupunguza Athari za Lugha ya Kijita Wakati wa Kuwasiliana kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili Sanifu

Lugha mama ni chanzo cha athari kwa wanafunzi walio wengi wa lugha ya Kiswahili sanifu kwa kiasi kikubwa. Matumizi ya lugha mama yaani Kijita kwa muda mrefu, Mwanafunzi huathiriwa sana katika kujifunza lugha nyingine kwa kuwa tayari anakuwa amekwisha kuwa na mazoea na lugha yake mama katika utamkaji wa sauti

za lugha hiyo. Mbinu za kuwasaidia kwa wale ambao tayari walishaathirika na lugha mama ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu ni hizi zifuatazo hapa chini: Kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza athari za kimatamshi na Kisitankisia kwa mwanafunzi aliyeanza shule na hivyo kumjengea uwezo wa kujiamini katika kutumia lugha ya Kiswahili kilicho sanifu na kinachoeleweka kwa watumiaji wengine wa lugha hii ya kiswahili sanifu katika kuzungumza na kuandika.

4.5.1 Mikakati ya Kupunguza Athari

Chanzo cha data ni kutoka kwa Watafitiwa Walimu, Wanafunzi na Wataalamu (Wazazi) waliojibu dodoso lililouliza ni mikakati gani inayofanyika ili kupunguza athari za lugha ya Kijita kwa wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Ili kupunguza athari za lugha ya Kijita inatakiwa kuwa na mazoea ya kuzungumza lugha ya Kiswahili sanifu katika mazingira yao ya shuleni ili Wanafunzi waweze kuzoea kuongea lugha hiyo bila usumbufu wowote wanapokuwa katika Mazingira ya nyumbani, badala ya kuongea lugha hii wanapokuwa shuleni tu. Pia ni kutumia lugha ya Kiswahili sanifu kwa upande wa Walimu wakati wa kufundisha somo hilo na kuzuia Wanafunzi kuongea lugha mama wawapo shuleni. Vilevile kuhimiza matumizi ya Kiswahili sanifu wawapo shuleni na nje ya shule (nyumbani), kuandaa chati yenye maneno mbalimbali ya lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kutumia kufundishia ili kusaidia wanafunzi walioathirika na lugha mama wakati wa ufundishaji. Kuwazoesha wanafunzi kuongea lugha ya Kiswahili muda wote. Kuwazuia wanafunzi kuongea lugha ya Kijita katika mzingira ya shuleni, kuwekewa mkazo katika ufundishaji wa somo hili la Kiswahili ili wasiwe na mazoea ya kuongea lugha ya Kijita wakati wa

ufundishaji, kuanza kuwafundisha lugha ya Kiswahili wakiwa wadogo.(kuazishwa) kwa madarasa ya shule ya awali hukohuko vijijini kabla ya kufikia umri wa kuanza shule ya msingi.

4.5.2 Matamshi ya Kiswahili

Matumizi mazuri ya matamshi katika mawasiliano huonesha uhusiano mzuri baina ya miundo ya lugha na mawasiliano. Chacha (2001) anaeleza kwamba nadharia ya mawasiliano ilikusudiwa kuimarisha mbinu za ufundishaji ambazo zitasisitiza uhusiano uliopo kati ya miundo ya lugha na mawasiliano. Katika swali la hojaji lililoulizwa kwa Watahiniwa Walimu kuwa je, ni athari zipi za kimatamshi zinazojitokeza kwa Wanafunzi wa Kijita wanapojifunza lugha ya Kiswahili? Utafiti huu ulionyesha kuwa endapo wataelekezwa vizuri, tatizo katika matamshi litapungua na pengine kwisha kabisa. Kama Habwe (2010) anasema, kwa muda mrefu elimu imetegemewa kama nguzo ya uhai wa Binadamu. Kila mtu na kila nchi imetafuta maarifa na kuzua mbinu mbalimbali za kujiboresha na kuiboresha Jamii kupitia lugha. Utekelezaji wa mambo haya yote umetegemea pakubwa mchango wa lugha. Lugha imekuwa nguzo muhimu katika hali zote shuleni na hata vyuo vikuu duniani kote kwa Maendeleo ya nchi nzima.

4.6 Kuwepo kwa Vikundi vya Kusoma na Mihadhara

Hii itasaidia sana kwa wale wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Data hii inatokana na swali la dodoso lililoulizwa kwa Watahiniwa Walimu kwamba. Usomaji wa vitabu vya hadithi, vipeperushi na Majarida vinavyohusiana na lugha ya Kiswahili. Je, vitasaidia wanafunzi wa Kijita katika kuboresha lugha ya Kiswahili? Utafiti huu ulibaini kuwa kwanza itawajengea uwezo mkubwa wa kuzungumza lugha

ya Kiswahili na hali ya kusimama mbele ya watu na kuzungumza bila uoga. Wanafunzi wengi wanakosa uwezo wa kuzungumza mbele za watu kutokana na kutokuwa na mazoea ya kuzungumza lugha ya kiswahili sanifu mbele ya watu ili kuendeleza mawasiliano. Musau (2001) mijadara, michezo, usomaji wa magazeti husaidia kuendeleza mawasiliano na kukuza lugha kwa wanafunzi mihadhara hii ikisha anzishwa katika shule za tarafa ya Nyanja, Wanafunzi wanaweza kuwa wazungumzaji wazuri wa lugha ya Kiswahili sanifu.

Utafiti huu ulikusudiwa kuwa ikiwa Wanafunzi watajengewa utamaduni wa kusoma vitabu vya ziada, Majarida, Hadithi na vipeperushi vinavyohusiana na lugha ya Kiswahili vitasaidia katika kuboresha lugha ya Kiswahili sanifu katika kuwasiliana. Usomaji wa vitabu na Majarida husaidia sana kwa Mwanafunzi katika kuelewa na kusaidia kujua lugha ya Kiswahili sanifu. Kuna faifa nyingi sana mwanafunzi aliyesoma majarida na vitabu anazipata, Mwanafunzi huwa Msomaji mzuri, pia humjengea hali ya kuwa na Msamiati mwingi, hujenga uwezo wa kujua kusoma kwa haraka. Kuwa na uwezo wa kutafasiri maneno ambayo ni magumu yaliyotumiwa katika habari na hadithi mbalimbali za Kiswahili, kuwa na uelewa jinsi ya kuunda sentensi mbalimbali za Kiswahili kama inavyostahili kutamkwa. Katika Jamii zilizo nyingi wanafunzi hawana utamaduni wa kujisomea vitabu vya hadithi na majarida ya Kiswahili. Katika Mazingira hayo mwanafunzi anapokosa umakini na umuhimu wa kuwa Msomaji mzuri wa kujiamini wa lugha ya Kiswahili. Hivyo hapana budi wanafunzi wa Kijita wajenge tabia na mazoea ya kusoma vitabu na majarida mbalimbali. Vitasaidia kuondoa athari ya kimatamshi katika mazungumzo yao ya kila siku.

Kiswahili ni lugha iliyo ya muhimu kwa wanafunzi wa Kijita kwa kuwa wengi wao wako karibu na Ziwa Victoria ambapo kuna changamoto za mwingiliano wa makabila mbalimbali katika shughulli za uvuvi. Hivyo kujua Kiswahili kutarahisisha mawasiliano kati yao na Jamii nyingine za kitanzania itasaidia kuwaunganisha katika Nyanja mbalimbali kwa kujuana na watu wengine, kusoma na kusikiliza taarifa zinazotolewa na vyombo vya habari mbalimbali vya ndani na nje ya nchi. Katika mikutano na makongamano yanayofanyika katika maeneo yao na nje ya pale walipo. Utafiti huu ni Watafitiwa Walimu, Wanafunzi na Wataalamu (Wazazi) walioona umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Kitanzania na jamii nyingine zinazotumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao. Kwa kuonesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili sanifu katika mawasiliano. Naye Chacha (2001) alibainisha lengo la nadharia ya mawasiliano kuwa ni kukuza uwezo wa kuwasiliana kama lugha ya Kiswahili ilivyo na umuhimu katika Tanzania.

4.7 Hitimisho

Katika sura hii utafiti umechanganua athari za Lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili. Utafiti umeonesha jinsi ambavyo kuna athari ya Lugha ya Kijita wakati wa kujifunza Lugha ya Kiswahili, utafiti umeonesha chanzo cha athari hizo kwamba ni kule kulazimisha mifumo ya lugha ya kwanza kwenda kwenye Lugha ya pili ambayo ni Lugha ya Kiswahili. Pia kuna hali ya kuchukulia Mazingira ya Lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili na hivyo kujikuta katika hali ya kuathiri Lugha ya pili. Pia utafiti umeona kuna suala la Walimu ambao ni wakijita au hata ambao siyo wajita kuitumia lugha hiyo ya kijita hata pale wanapokuwa shuleni na hivyo kumfanya

Mwanafunzi kuendelea kutumia Lugha hiyo na kushindwa kuona tofauti iliyopo kati ya Mazingira ya nyumbani na shuleni. Ushauri ni kwamba ni vema Walimu watumie Lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi wao wawapo shuleni. Hii itafanya kuinua hali ya Lugha hii kwa Wanafunzi, utafiti pia umeona kuwa ili kuinua kiwango cha Lugha hii ya Kiswahili kwa Wanafunzi pana haja ya kuanza kuitumia na kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa ya mawasiliano hata pale wanapokuwa nyumbani ili wanapoanza shule wawe tayari wana uelewa juu ya Lugha ya Kiswahili na hivyo kurahisisha suala zima la ujifunzaji na ufundishaji kwa hawa Wanafunzi. Katika utafiti huu imebainika kuwa pana udhaifu wa sheria shuleni ambapo Wanafunzi wanatumia Lugha mama (ya Kijita) bila kuwa na shaka yoyote wawapo shuleni na hakuna ufuatiliaji kutoka mamlaka za shule zinazohusika na udhibiti wa Lugha mama wawapo shuleni na hivyo kumafanya Mwanafunzi asione tofauti ya shuleni na nyumbani kwani bado anaendelea kutumia lugha hiyo hiyo ya kwanza hivyo hapana budi mamlaka zinazohusika kuzingatia sheria za kumfanya Mwanafunzi kuzungumza Lugha ya Kiswahili awapo shuleni ili ajengewe Mazingira ya kuongea lugha ya Kiswahili hata awapo nyumbani.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii ilifanya Muhtasari, Mapendekezo na Hitimisho ya Utafiti mzima. Utafiti huo ulilenga kujua athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu kwa ujumla umeweza kujibu maswali yaliyokuwa yameulizwa katika sehemu ya malengo mahsusi. Utafiti umeweza kujibu hoja ya utafiti kuwa pana athari kwa wanafunzi wa kuhamisha uzoefu kutoka lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili ambaloni tatizo kubwa kwa wanafunzi wa kijita katika shule za Msingi ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili Sanifu. Tatizo hili linatokana na mazingira ya shule kutoweka misingi na mikakati iliyo mizuri kwa mwanafunzi anapokuwa katika eneo la kujifunzia (Shuleni), hivyo kushindwa kuona utofauti kati ya nyumbani alikotoka akiongea lugha ya Kijita na shuleni anapopaswa kubadilisha lugha kwa kutumia lugha ya Kiswahili Sanifu muda wote awapo shuleni. Kwahiyo panahaja ya kuwajengea mazingira mazuri ya kujifunzia na kusomea wanapokuwa shuleni ili watumie lugha ya kiswahili kwa wakati wao wote wa kujifunza shuleni.

5.3 Mapendekezo

Walimu wale ambao ni wakijita na wale ambao sio wajita wasitumie lugha hiyo ya Kijita kuwasiliana na wanafunzi wawapo darasani au nje ya darasa, hii itawajawenmgea wanafunzi uzoefu na uwezo wa kuwasiliana wao kwa wao wawapo shuleni na pia wawapo nje ya shule kwa lugha ya Kiswahili Sanifu. Walimu wafanye utaratibu wa kuanzisha vikundi ambavyo vitafanya wanafunzi waweze kuwa katika vikundi vyao watakavyokuwa wamevianziasha. Pawepo na sheria za shule za kuiwafuatilia wale wote wanaotumia au kuongea lugha ya kijita wawapo darasani au nje ya darasa wanafunzi wakimuydu kuongea lugha hii ya kiswahili sanifu shuleni itawasaidia kuwasiliana kwa Kiswahili Sanifu hata watakapo kua nyumbani ,kwani

tayari wanauzoefu wa kutosha kuongea lugha hii ya Kiswahili Sanifu bila shida wakiwa shuleni. Pia itakuwa ni vizuri zaidi kama mashirika na taasisi mbalimbali za uendelezaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu kama SIKILUKI, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) pamoja na vyombo mbalimbali vya habari vilevile na vya mashirika mbalimbali ya Kiswahili wakahamasisha matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili Sanifu, pamoja na kujitokeza wafadhili tofauti tofauti ambao watawafadhili watafiti katika utafiti wao ambao watajishughulisha na uchunguzi huo.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu kwa ujumla umefanikiwa kufumbua kiini cha tatizo la athari ya lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu kwa Wanafunzi wa shule za Msingi Wilaya ya Butiama Tarafa ya Nyanja, Mkoa wa Mara kuwa ni tatizo linalosababishwa na baadhi ya mambo kadha wakadha.

Kwamba Wanafunzi wa shule za Msingi hutumia lugha ya Kijita katika Mawasiliano yao. Wanafunzi hutumia kijita wawapo nyumbani kuwasiliana na Wazazi wao. Pia hawa Wanafunzi wanapokuwa shuleni hutumia Kijita kuwasiliana wao kwa wao hili ni tatizo kubwa kwa hawa Wanafunzi. Hivyo ili kupunguza tatizo hili ni vema Serikali na wadau wengine watilie mkazo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu, Wanafunzi waelekezwe juu ya matamshi sahihi ya lugha ya Kiswahili sanifu, na kuanzishwa kwa Makongamano, Midahalo na semina mbalimbali zinazohusiana na Kiswahili sanifu katika shule zote za Msingi na Sekondari.

Hivyo ili kupunguza tatizo hili ni vema uongozi wa shule katika shule husika wakaanzisha vikundi mbalimbali vya kimasomo na kuweka mkazo wa kuzungumza lugha ya kiswahili kwa wanafunzi wote wanapokuwa ndani ya madarasa na nje ya madarasa ili kuweza kuinua hali ya kiwango cha kuweza kuongea lugha ya kiswahili sanifu wanapokuwa katika mazingira ya shule na nje ya mazingira ya shule. Pia kila shule iwe na utaratibu wa kuwa na shule ya awali ambayo wanafunzi wa chekechea wataanza kufundishwa kuongea lugha ya kiswahili sanifu wakiwa wadogo na hivyo kuwajengea uwezo wa kumudu kuongea lugha ya kiswahili sanifu wakiwa watoto wadogo. Walimu watumie lugha ya Kiswahili sanifu mda wote wanapowasiliana na wanafunzi wao. Hivyo kutafanya wanafunzi waige kuwasiliana kwa kuiga kutoka kwa walimu wao kwa kutumia kiswahili. Hili litafanikiwa kama shule katika maeneo hayo watakuwa na utaratibu huo.

MAREJELEO

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Corder, S. P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage*, Oxford: Oxford University press.

- Enon C. J. (1995). *Educational Research Statistic Measurement*. Kampala: Makerere University Press.
- Habwe J. H na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Nairobi Phoenix Publishers.
- Kipacha, A. (2007). *OSW 101 Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
- Kothari, R. C. (2014). *Research Methodology Methodes and Techniques 3rd edition*, New Delhi: New age International (P) Ltd.
- Massamba, D. P. B (2007). *Kiswahili orignal and Bantu Divergence corvergence*. Dar es Salaam: Theory Institute of Kiswahili Reseach.
- Massamba D. P. B. (2009). *Kamusi ya Isimu na falsafa ya lugha*, Dar es Salaam: TUKI Publication.
- Matinde, (2012). *Dafina ya lugha, Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mbogo S. (2012). *Research Methodology*. Dar es Salaam: The Open University of Tanzania
- Mdee J. S. (2013). *Kamusi ya Karne ya 21*. Kenya, Uganda, Tanzania. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Mdee J.S. (Mwaka haujulikani) OSW 613 Isimu Jamii chuo kikuu huria cha Tanzania Dar es salaam.
- Mekacha. R.D. K. (2000) *Isimu Jamii: Nadharia na Mukdadha wa Kiswahili*. Osaka University of foreign studies.
- Msanjila Y. P. na wenzake (2009) *Isimu Jamii*. TUKI Dar es salaam.

- Mussau, Paul M. Chacha, Leonard M. (2001) Mbinu za kisasa za kufundishia Kiswahili upili na vyuo, Nairobi, Kenya Literature Bureau.
- Nyandago, F.O. (2013) Uchanganuzi linganishi wa Sintaksia wa sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Obara. J. M. (2014), Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na Wanafunzi wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Otiende, M. A. (2013) Athari za mofolojia ya Kibasuba katika matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya pili. Tasnifu ya M.A. (UON).
- Paul. M, Msau, Leornard M, Chacha (2001) Mbinu za kisasa za kufundisha Kiswahili na vyuo. Nairobi Kenya. Literature Bureau.
- Raponda, M.M (2005) Makosa ya Kimofosintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule ya Upili Jijini Nairobi. Tasnifya M.A. (UON).
- Rocha (2011) Kiswahili Past Present and Future horizon. Nairobi Uniersity Press.
- Selinker, L. (1969) Language transfer, General Linqustics New York: Raw hence Eribaum Associates, inc (RAL)
- Serlinker (1972) Interlanguage. New York. Rawlence. Eribaum Associates, inc. (RAL).
- Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (2004) Kamusi ya Kiswahili sanifu. Oxford University press Dar es salaam.
- Tonya, L.M (1978) Misingi ya Kiswahili Muhenga Publishing Consultants Company Ltd.

TUKI, (2004) Kamusi ya Kiswahili sanifu. TUKI: Oxford Univerty Press East Africa
Ltd. Kenya.

Yule George (2010) the study of language. Cambrige Univeristy place.

VIAMBATANISHO

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII

IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI

Kiambatanishi 1: Dodoso Kwa Walimu

Sehemu A: Utangulizi.

Mimi ni Mwanachuo wa Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo ninasoma Kiswahili Isimu. Ninafanya utafiti kuhusu athari za Kiisimu za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu katika Shule za Msingi Chimati A na Bulinga A katika darasa la tano hadi darasa la saba zilizoko Wilaya ya Butiama Mkoani Mara. Dodoso hili linalenga kukusanya na kupata majibu ya utafiti utakao msaidia Mtafiti kuboresha na kupata mwelekeo wa Utafiti wake. Majibu utakayoyatoa yatakuwa ni siri na yatatumika katika Utafiti huu tu na si vinginevyo:

Sehemu B: Maelezo kuhusu Mtafitiwa.

Taarifa za awali za Mtafitiwa

Jina _____

Umri _____

Jinsia _____

Kiwango cha Elimu _____

Sehemu C: Maswali Yanayolingana na Utafiti

1. Wewe ukiwa Mwalimu wa Shule ya Msingi Chimati A/Bulinga A lugha yako mama ni ya Kijita? _____

2. Ikiwa wewe ni Mjita taja athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu _____
3. Je, Wanafunzi wanapokuwa nyumbani wanatumia lugha ipi katika Mawasiliano na Wazazi wao?
- (a) Lugha ya Kijita
- (b) Lugha ya Kiswahili
- (c) Majibu yote ni sahihi ()
4. (a). Je, Wanafunzi wa Shuleni kwako wanazungumza Kiswahili sanifu? _____
- (b) Kama ni hapana athari zipi zinajitokeza?

Orodhesha

5. Kiisimu ni maneno gani ya lahaja ya Kijita yanayoathiri matamshi ya Lugha ya Kiswahili.

Orodhesha

6. Ni mikakati gani inayofanyika ili kupunguza athari za lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu?

7. Je, Mazingira yanaweza kuwa ni sababu moja wapo ya kuwaathiri Wajita katika kujifunza lugha ya Kiswahili?

- (a) Ndiyo (b) Hapana ().

8. Usomaji wa vitabu vya hadithi, vipeperushi na Majarida vinavyohusiana na lugha ya Kiswahili. Je, vitasaidia watoto wa Kijita katika kuboresha lugha ya Kiswahili sanifu?

(a) Ndiyo (b) Hapana ()

9. Je, Matumizi ya lugha zaidi ya moja katika Jamii husababisha mwingiliano katika Msamiati wa lugha katika Jamii husika?

Jedwali.4.1

Idadi ya Watafitiwa	Kiswahili	Kijita

10. Andika maneno yafuatayo kama nitakavyo kusomea.

- i) Dhambi.....
- ii) Lafudhi.....
- iii) Dhahabu.....
- iv) Dhumuni.....
- v) Adhabu.....

Soma maneno yafuatayo kama yalivyoandikwa

- i) Dhambi.....
- ii) Lafudhi.....
- iii) Dhahabu.....
- iv) Dhumuni.....
- v) Adhabu.....

Swali la hojaji

11. Je, ni athari zipi zinazojitokeza kwa Wanafunzi wa Kijita wanapojifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

Ahsante kwa Ushirikiano wako

Kiambatanishi 2: Dodoso kwa Wanafunzi

Sehemu A: Utangulizi.

Mimi ni Mwanachuo wa Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo ninasoma Kiswahili Isimu. Ninafanya Utafiti kuhusu athari za kiisimu za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu katika Shule za Msingi Chimati A na Bulinga A zilizoko Wilaya ya Butiama Mkoani Mara. Dodoso hili linalenga kukusanya na kupata malengo ya Utafiti utakaomsaidia Mtafiti kuboresha na kupata mwelekeo wa Utafiti wake. Majibu utakayo toa yatakuwa ni siri sana na yatatumika katika utafiti huu tu na si vinginevyo.

Sehemu B: Maelezo kuhusu Mtafitiwa.

Taarifa za awali za Mtafitiwa

Jina _____

Umri _____

Jinsia _____

Kiwango cha Elimu _____

Sehemu C: Maswali yanayolingana na Utafiti

1. Je, lugha mama ni lugha gani? Ipi ni lugha mama kati ya Kijita na Kiswahili.

2. Ni lugha ipi unayotumia katika Mawasiliano ukiwa:-

(a) Nyumbani _____

(b) Shuleni _____

3. Je, unapotumia lugha zaidi ya moja, mfano Kijita, Kiswahili au Kiingereza kuna athari zozote zinazojitokeza?

(a) Ndiyo (b) Hapana (c) Hakuna jibu ()

Tetea hoja zako kulingana na jibu ulilochagua.

12. Orodhesha maneno matano (5) ambayo yanaonyesha athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu:-

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(iv) _____

(v) _____

13. Ni mikakati gani inayotakiwa kufanyika ili kupunguza athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

14. Je, ni sababu gani zinazochangia kuwaathiri Watoto wa Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu wawapo shuleni?

Jedwali 4.2

Idadi ya Wanafunzi	Kiswahili	Kijita

15. Athari zipi zinajitokeza wakati wa kujifunza lugha ya Kiswahili kwa Watoto wa Kijita?

Jedwali 4:3

Maneno ya Kiswahili	Vitamkwa vinavyoongezwa na Wazungumzaji wa Kijita

(i)	(i)
(ii)	(II)
(iii)	(iii)
(iv)	(iv)

Swali la Hojaji.

16. Je, ni athari zipi za kimatamshi zinazojitokeza kwa Wanafunzi wa Kijita wanapojifunza lugha ya Kiswahili?_____

Ahsante kwa Ushirikiano wako

Kiambatanishi 3: Dodoso kwa Wataalamu (Wazazi) Walugha ya Kijita

Sehemu A: Utangulizi.

Mimi ni Mwanachuo wa Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo ninasoma Kiswahili Isimu. Ninafanya Utafiti kuhusu athari za Kiisimu za lugha ya Kijita katika Kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu katika Vijiji vya Chimati na Bugunda vilivyoko Wilaya ya Butiama Mkoani Mara. Dodoso hili linalenga kukusanya na kupata majibu ya utafiti utakao msaidia Mtafiti kuboresha na kupata mwelekeo wa Utafiti wake. Majibu utakayo yatoa yatakuwa ni siri sana na yatatumika katika Utafiti huu tu na si vinginevyo.

Sehemu B: Maelezo kuhusu Mtafitiwa.

Taarifa za awali za Mtafitiwa

Jina _____

Umri _____

Jinsia _____

Kiwango cha Elimu _____

Sehemu C: Maswali yanayolingana na Utafiti

1. Je, Wazazi wanatumia lugha ipi katika kuwasiliana na Watoto wao wanapokuwa nyumbani?

(a) Kiswahili

(b) Kijita ()

Kama jibu ni Kijita toa sababu au kama ni Kiswahili pia toa sababu

2. Kwa nini Wanafunzi wameathiriwa na Lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili? _____

Fafanua kwa kutumia mifano kuntu

3. Je, Wewe ni Mzawa wa lugha ya Kiswahili au lugha hii ni lugha ya pili kwako?

(a) Ndiyo (b) Hapana ()

4. Orodhesha maneno matano (5) ambayo yanaonesha athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu.

- (i) -----
- (ii) -----
- (iii) -----
- (iv) -----
- (v) -----

5. Maneno yafuatayo hutumika katika lugha ya Kijita yana maana gani katika lugha ya Kiswahili sanifu?

- (a) Angaliapo _____
- (b) Nendako _____
- (c) Tazamapo _____
- (d) Chunguliapo _____
- (e) Chezapo _____

6. Ni mikakati gani inayotakiwa kufanyika ili kupunguza athari za lugha ya Kijita katika kujifunza Lugha ya Kiswahili sanifu?

7. Je, kufundisha Watoto lugha ya Kiswahili tangu Utotoni kutasaidia kuondoa athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili?

Jedwali 4:5

Ndiyo	Hapana

8. Nini pendekezo lako kuhusu mawasiliano kwa kutumia lugha ya Kiswahili katika familia za Kijita?

Swali la hojaji

9. Wewe ukiwa Mzazi wa Mwanafunzi unajukumu gani kusaidia kuondoa athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

Ahsante kwa Ushirikiano wako